Gazeti la kwanza la Kiislam kutolewa kwa lugha ya Kiswahili - mwaka 1936

Mapenzi ya Mungu

Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote

DAR ES SALAAM TANZANIA

JUZU 74 No. 180 | SHAWWAL 1435 AH | AGOST 2014 | ZAHOOR 1393 HS | BEI TSH. 500/=

Nukuu ya Qur'an Tukufu

Hakika Tumeiteremsha (Qur'an) katika usiku wa heshima.
Na nini kitakujulisha usiku wa heshima ni nini?
Usiku wa heshima ni bora kuliko miezi elfu.
Huteremka humo malaika na roho wakiwa na agizo la Mola wao kuhusu mambo yote.
Amani - na itakuwa hivyo mpaka mapambazuko ya alfajiri.

(*Al- Qadr* 97 : 2 - 6).

Khalifatul Masih awaasa Waislamu duniani:

Bila Umoja hakuna Lailatulqadir

Na Mwandishi wetu, London

Amirul Muuminuun (Kiongozi wa Jumuiya ya Waislamu Waahamdiyya duniani) Hadhratul Mirza Masroor Ahmad, Khalifatul Masih V a.t.b.a. katika hotuba yake ya Ijumaa ya mwisho wa mwezi wa Ramadhani 2014 alisema:

Siku kumi za mwisho za Ramadhani zinapita upesi. Waislam wanayapa uzito mambo mawili katika siku hizi kumi za mwisho, moja ni *Lailatul Qadir*, usiku wa hatima na jingine ni *Jumatul Wida*, ijulikanayo kama Ijumaa ya kuagana. Umuhimu wa Usiku wa hatima ni jambo la kweli kama lilivyothibitishwa na Hadithi na vilevile Qur'anTukufu. Hata hivyo dhana ya Ijumaa ya kuagana ni jambo ambalo Waislam au wanavyuoni wamelibuni kupitia tafsiri zao wenyewe ambazo si sahihi.

Hadhrat Khalifatul Masihi alitoa maelezo kuhusu mambo haya mawili, hii leo na akatoa kipande cha hotuba ya Ijumaa ya zamani ya Hadhrat Musleh Mauud, (Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad) (ra) kuhusiana nayo.

Muhadithina mbalimbali wa Hadithi wanatoa tarehe tofauti tofauti kwa usiku wa hatima, baadhi wanasema ni usiku wa mwezi 21, wengine wanasema ni usiku wa 23 wa Ramadhani wakati wengine wanasema wana hakika ni usiku wa 27.

Kwa vyovyote vile hadithi zinasema usiku huo utafutwe katika siku kumi za mwisho za ramadhani. Mtume Mtukufu (saw) alipewa elimu ya tarehe maalumu ambayo usiku wake Mwaminio wa kweli hushuhudia upokelewaji maalum wa maombi. Hata hivyo, Hadithi zinatueleza kwamba kwa sababu ya makosa ya Waislam wawili Mtume Mtukufu (saw) alisahau tarehe hiyo maalum. Halikuwa ni jambo la kawaida kuifahamu mahsusi tarehe hiyo na ilikuwa daima ni hamu ya Mtume Mtukufu (saw) kuwajulisha habari hii Waaminio. Hadithi zinatuambia kwamba baada ya kuipata elimu hii Mtume Mtukufu (saw) alitoka nyumbani kajawa furaha ili awajulishe watu habari hii lakini hapo nje akakutana

Endelea uk. 3

Majibu kwa Gazeti la Alhudaa

• *Mhariri wake abuni Kalima Mpya, ashindwa kutafakari, Je mwendawazimu aweza kutolewa kutoka kwenye Uislamu?*

SEHEMU YA 1

Na Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Mhariri wa gazeti la Al Hudaa toleo namba 470 la tarehe 24 – 30 July 2014 sambamba na siku ya Alkhamisi ndani ya mwezi mtukufu wa Ramadhani wa mwaka 1435 Hijriyya, alianza makala yake ya uhariri kwa kuandika:

Mwasisi, viongozi, na wafuasi wa Ahmadiyya si Waislamu. Hii ni kufuatia tamko la Maulamaa wa Kiislamu katika nchi zote za Kiislamu Duniani. Mwislamu ni yule tu anayeitakidi kuwa hakuna Mungu isipokuwa Mmoja tu, Ambaye ni Allah au Mwenyezi Mungu Mtukufu na Muhammad saw ni Mtume Wake wa Mwisho:

Kauli hii inapinzana moja kwa moja na kauli ya yule aliyetuletea dini hii ya Islamu toka kwa Mwenyezi Mungu, yaani Mtume Muhammad saw.

Siku moja Mtume Muhammad saw alipokuwa ameketi sehemu fulani na Masahaba wake ra, alitokewa na Malaika Jibril a.s., aliyeonekana na wote waliojumuika hapo, akiwa amevaa mavazi meupe sana. Jibril alimuuliza Mtume saw kwamba Islam ni nini, na Mtume saw akamjibu kuwa ni kushuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah na Muhammad ni Mtume wake. Kusali sala tano, kutoa Zaka, kufunga Ramadhani na kuhiji Kaaba. Kila Mtume saw alipokuwa akijibu, Malaika Jibril alikuwa akimsadikisha kwa kumwambia Swadaqta, yaani umesema kweli.

Kwa hiyo, kwa kauli hiyo ya Mtume saw, iliyosadikishwa na Malaika wa Mwenyezi Mungu, aliyetumwa makhsus katika hafla hiyo kuja kuufundisha Uislamu wa kweli, mwislamu wa kweli ni yule anayeshuhudia kuwa hapana apasaye kuabudiwa ila Allah na kushuhudia kuwa Muhammad ni Mtume wa Allah. Masheikh wa gazeti la Alhudaa wamepachika neno wa mwisho ili kalima iwe ikisomeka Mtume wa mwisho wa Allah, badala ya Mtume wa Allah.



Sheikh Bakri Abedi Kaluta

Kwa rai hiyo ya Masheikh wa Alhudaa, mtu hawi mwislamu kwakuyaaminina kuyatekeleza yale yaliyobainishwa na Mtume Muhammad saw na kusadikishwa na Malaika wa Mungu, bali ni sharti awe pia mwenye kukiamini na kukitekeleza kile kilichobandikwa na Masheikh hao wa gazeti la Alhudaa.

Waislamu wa Ahmadiyya wanaamini na kutekeleza yale yote yaliyobainishwa na Mtume Muhammad saw na kusadikishwa na Mwenyezi Mungu kupitia Malaika Wake Jibril. Kama madai ya Masheikh wa Alhudaa ni sahihi kwamba, Waahmadiyya, juu ya kuyaamini na kuyatekeleza yote hayo, bado wanakuwa sio Waislamu, basi itabidi watu wakiri kwamba Mtume saw (Mungu Apishe mbali) alisema uongo na Malaika Jibril hakuwa mkweli alipomwambia Mtume saw kuwa amesema kweli.

Kwa hiyo kila mwenye akili timamu, busara na uchaMungu anayo hiari ya kuchagua kauli ya Mtume saw yenye ushuhuda wa kimbingu, ambayo imewajumuisha Waahmadiyya ndani ya

Endelea uk. 4

Mapenzi ya Mungu

Maoni ya Mhariri

Vyombo vya habari vya Kiislam

Katika siku za mwanzo za dini tukufu ya Islam maadui walikwenda mbali mno katika dhamira yao ya kuifutilia mbali dini tukufu ya Islam kwenye uso wa ardhi. Walishika silaha ili kuiangamiza Islam nao Waislamu wakashika silaha ili kuilinda.

Maadui wa Islam bado wanaendelea na vita vyao hadi hivi leo. Lakini safari hii wamekuja na mbinu mpya. Wanatumia zaidi kalamu. Kalamu imetumika sana katika kuidhalilisha dini tukufu ya Islam, kuyapotosha mafundisho ya dini tukufu ya Islam na kutoa taswira ambayo sio sahihi hata kidogo. Hivi leo usione ajabu hata kidogo kusikia ikielezwa ya kwamba Islam si kingine chochote isipokuwa ugaidi. Kalamu imetumika vibaya sana lakini kalamu inayoshika msitari wa mbele ni ile inayohusiana na magazeti na luninga. Bila shaka katika vita hii Waislamu nasi tunahitaji kuitumia kalamu kiusahihi kabisa!

Katika nchi yetu kwa muda mrefu hatukuwa na chombo cha habari kinachonasibishwa na Islam. Ni mwaka 1936 ndipo tulipopata chombo cha kwanza cha habari kinachomilikiwa na Waislamu. Chombo hicho kilijitahidi sana kufuata maadili yote ya Islam kwa kuelimisha na kutoa habari za kusaidia jamii iende mbele. Kwa miaka yote chombo hicho hakikujishughulisha hata kidogo katika kuigawa au kufitinisha jamii. Kwa msaada mkubwa sana wa Mwenyezi Mungu hivi leo tunavyo vyombo vingi vya habari katika nchi yetu vinavyomilikiwa na waislamu. Hivyo tunatarajia ya kwamba vyombo hivyo navyo vitafanya kazi ambayo ni kutoa taswira sahihi ya dini tukufu ya Islam.

Hata hivyo kwa masikitiko makubwa, hivi karibuni vyombo vya habari vya kiislamu vimegeuka kuwa uwanja wa kukebehiana kusutana na kudhalilishana. Tabia zote hizi hazina uhusiano wowote na dini tukufu ya Islam. Bila shaka tunayo mengi sana ya kufanya ili kutoa mafundisho ya dini tukufu ya Islam kwa jamii. Hivyo hatuna nafasi hata kidogo ya kutoshughulikia swala la msingi ambalo ni kufikisha mafundisho ya Quran tukufu na kueleza mwenendo wa Mtume Mtukufu s.a.w. Tunatumaini ya kwamba tutajitahidi kujirekebisha sisi sote na kufuata kanuni za msingi za uandishi wa habari ambazo kwa hakika ndio Uislamu wenyewe - yaani kusema kweli na kujitahidi kufanya utafiti kabla ya kuandika jambo lolote.

Ndani ya Qur'ani tukufu Mwenyezi Mungu Ameonya juu ya wale wasiosema kweli kwamba ni sawa na waabudu masanamu na pia wale wanaosema mambo wasiyo na elimu nayo, kwamba masikio yao na macho yao na nyoyo zao vitaulizwa.

Tunadhani hata heshima ya gazeti inapungua mno wakati linapotoa habari ambazo hazijafanyiwa uchunguzi na ambazo si sahihi hata kidogo na ambazo hazihitaji uwe ni dhehebu gani ili kuuona upungufu wake.

Kwa mfano kama gazeti litazungumzia ya kwamba nchi ya Tanganyika ilipata uhuru mwaka 1910 sio tu kwamba litakuwa limekosea bali ni dhahiri ya kwamba utafiti haukufanywa.

Sasa tafakari, katika magazeti ya Kiislamu hapa nchini, liko moja lililowahi kuweka picha ya Kiongozi Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya duniani Hadhrat Mirza Masroor Ahmad a.t.b.a, lakini gazeti hilo likaandika kwamba huyu ni William Montgomery. Watu tukabaki vinywa wazi, tukiwa tumepigwa butwaa!

Nalo gazeti jingine la Kiislam lilishawahi kuandika mwaka aliozaliwa mwanzilishi mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya ambao sio mwaka sahihi kabisa!

Hivi karibuni gazeti moja tena likaandika makala iliyokuwa na kichwa kizito *'Makadiani waficha dawa za kulevywa kwenye magunia ya Mchele'*! Lakini ukiisoma makala hiyo haina kichwa wala miguu, haina uthabiti wowote bali haihusiani na hapa kwetu na tena eti ni tukio la miaka ya 90. Ni habari iliyoandikwa ovyo ovyo na bila shaka yoyote anayesoma kwa kina anajua kwamba habari hiyo haikufanyiwa utafiti wowote!

Tunadhani, bila kujali tofauti za kiimani na za kimadhehebu ni vyema waandishi wa vyombo vya kiislamu wakajikita kwenye kuandika habari za kweli na zilizofanyiwa utafiti wa kina ambazo ndizo sifa muhimu za Muislamu. Kwani mbali na kujivutia ghadhabu ya Mwenyezi Mungu kwa tabia ya kutokusema kweli na kuandika usiyo na elimu nayo, tabia hiyo pia inavifanya vyombo vya kiislamu vidharaulike mbele ya dunia na kuonekana waandishi wake ama ni majuha au mbumbumbu!

Tukumbuke kauli moja maarufu ya uandishi wa habari kwamba: ***Bila ya utafiti huna haki ya kaundika!***

Jalsa Salana, historia, shabaha na baraka zake

Na Waseem Ahmad Khan
Tabora

Mtume wetu Mtukufu Seyydna Hadhrat Muhammad Mustafa saw alisema ya kwamba hakika kuna baadhi ya malaika watukufu wa Allah wazungukao ili kutafuta mikutano ambamo Allah na Mtumewakehutajwahumo,basi wanapokuta mkutano wa aina hii,huwa wanakaa pamoja nao,na kufunika wenzao kwa mabawa yao na baadaye humweleza Allah hali ya mkutano huo.Washiriki hao wa mikutano hii hupata Baraka nyingi zitokazo kwa Mola wao hata hivyo mwenye kukaa nao bila kutia uzito jambo hilo pia hakosi Baraka zake,bali naye vilevile husamehewa na Allah Karim.

Kwa fadhila na msaada maalum wa Allah,sisi wafuasi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya tumejaaliwa kuwa na mkutano mtakatifu wa aina hiyo ambao hufanyika katika nchi zote ambapo jumuiya ipo na ni sehemu muhimu kati ya mipango inayofanyika kwa mwaka mzima.Tunaweza kuitaja kuwa MKUTANO WA KITAIFA au JALSA SALANA.

Mwanzilishi Mtukufu wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya Syedna Ahmad as alianzisha Jalsa Salana kwa idhini ya Mwenyezi Mungu na mkutano wa kwanza uliofanyika mnamo mwaka 1891 ulihudhuriwa na wafuasi 75.Syedna Ahmad as akielezea umuhimu wa mkutano huu alisema,mkutano huu msiuchukulie kama mikutano mingine ya dunia bali hili ni jambo ambalo msingi wake umewekwa na Allah naYe Ameyatayarisha mataifa ambayo hivi karibuni yatakuja kuungana nayo.

Alisema kwa imani ya hali ya juu na kwa jalali ya kwamba msiyadhani mambo haya hayawezekani,kwa kuwa hiki ni kitendo cha Mweza Yule Ambaye hakuna jambo lisilowezekana mbele yake.

Jambo hili la Allah lilitimia barabara na hakuna yeyote aliyeweza kulisitisha hilo. Jumuiya iliendelea kuenea pembezoni mwa dunia na watu wa mataifa mbalimbali waliendelea kuingia katika jumuiya makundi makundi,washiriki wa Jalsa Salana nao waliendelea kuongezeka,hivyo mkutano wa mwisho uliofanyika katika maisha matakatifu ya Syedna Ahmad as mnamo mwaka 1907 watu walioshiriki katika mkutano huo walikuwa 3000. Baada ya kufariki kwa Syedna Ahmad as ukhalifa ulipatikana katika jumuiya na chini ya uongozi huo jumuiya iliendelea kupata maendeleo siku hadi siku na ujumbe wa Islam kwa kupitia jumuiya ulifika duniani kote na pale ambapo ujumbe ulifika na jumuiya kustawi huko nidhamu ya Jalsa Salana ilianzishwa kwa lengo la kuwalea na kuwaelimisha wanajamaati wa nchi husika. Kama nilivyosema kuhusu idadi ya washiriki wa Jalsa,jinsi walivyoongezeka ieleweke ya kuwa mkutano wa mwaka 1983 uliofanyika katika makao makuuyaJumuiyamjiniRabwah Pakistan,watu wasiopungua Laki Tatu walihudhuria mkutano huo,jambo ambalo liliwatetemesha viongozi wa serekali pamoja na masheikh wa kijina wa kiislamu akiwemo rais wa nchi Jenerali Muhammad Zia ul Haqq wakawa tayari kuchukua hatua kali dhidi ya Jumuiya na kuimaliza mara moja.Wapinzani hao pamoja na kuchukua hatua ya kupiga marufuku juu ya mkutano wa jumuiya walitengeneza njama ya kuuangamiza ukhalifa lakini LINALOPANGWA NA ALLAH BILA SHAKA YOYOTE KUTIMIA NI WAJIBU,siku nyingi kabla ya kupigwa marufuku juu ya mkutano wa Jumuiya nchini Pakistani mti huu mtakatifu wa Jalsa Salana ulikuwa umekwishapandwa katika nchi mbali mbali duniani na mizizi yake ilikuwa imekwishastawi imara mno.Upande mmoja Jalsa Salana ilianzishwa huko Indoneshiya na upande mwingine msingi wake uliwekwahukoGhana,mkutano ulipofanywa Marekani basi nchini Uingireza na Ujerumani mikutano ya aina hii ilianza kufanyika na hali ya sasa ndiyo hii ya kwamba kwa fadhila na msaada maalum wa Allah katika maeneo ya mashariki na magharibi,kusini na kaskazini ilmuradi katika sehemu mbalimbali ya dunia mpango wa Jalsa Salana umekuwa sehemu maalum ya kalenda ya Jumuiya na jambo lisemwalo na Masihi na Mahdi wa Mtume Muhammad saw linatimia kwa shani yake pekee,ya kuwa kila taifa litakunywa maji toka chemchem hii.Licha ya kuwa na rangi na makabila tofauti mataifa mbalimbali ya dunia yanaendelea kujifaidisha na silsila hiyo.

Jalsa Salana,iwe ikifanyika katika bara yoyote ya dunia ina rangi moja na shani yake isiyokuwa na kifani,na washiriki wa Jalsa hiyo hupata Baraka nyingi zilizomo pamoja na sehemu ya kutosha ya maombi yaliyofanywa na Syedna Ahmad as kwa ajili wa washiriki hao wote.

Syedna Ahmad as kwa kuelezea shabaha ya kuanzishwa kwa Jalsa Salana alisema yakuwa katika mkutano huu elimu na mawaidha mbalimbali yatatolewa ambayo ni muhimu kwa ajili ya kuendeleza na kuongeza imani,yakini na maarifa,pia watakaoshiriki wataombewa dua maalum mbele ya Allah ili Allah Awakubali hao na kuwapa mabadaliko matakatifu katika maisha yao vilevile faida nyingine ipatakanayo ndiyo hii ya kuwa kila mwaka ndugu wapya watakaojiunga na jumuiya hiyo,kwa kuhudhuria mkutano huo wataweza kukutana na ndugu zao wa zamani na kwa kufanya hivyo mahusiano ya udugu na mapenzi yataongezeka na ndugu atakayetangulia mbele ya haki katika muda huu ataombewa dua maalum katika mkutano huu na kwa lengo la kuwaunganisha ndugu wote wa kiroho na kuondoa ugeni na unafikii kati yao itafanywa juhudi maalum na wale ambao wana uwezo mdogo wa kiuchumi inawapasa kuwa na mpango wa kuhudhuria Jalsa Hii na endapo kwa kufanya mpango na kutumia busara wataanza kuweka akiba kwa ajili ya matumizi ya Jalsa kila siku au kila mwezi na kuweka pembeni basi bila kuwa na shida yoyote wataweza kuwa na matumizi ya safari ya Jalsa.

Ndugu wasomi Jalsa Salana ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ni ushahidi wa kweli wa jumuiya na ni kioo kinachonesha shani ya jumuiya na wanajumuiya kwa jumla.Ingawaje jalsa salana ya jumuiya ya waislamu wa ahmadiyya Pakistan ilipigwa marufuku mwaka 1984 lakini mwaka huo huo Hadhrat Khalifa tul Masihi wa nne ra alihamia Uingireza na mwaka 1985 mkutano uliofanyika huko Uingireza ulipata sura ya mkutano wa kimataifa kwa sababu ya uwepo wa Ukhalifa nchini humo,ni mkutano ambao una umuhimu wake pekee kwani Khalifa Mtukufu wetu anashiriki na kutoa hutuba mbalimbali na kila mwaka mkutano huo unapata maendeleo makubwa katika pande zote pamoja na hayo Khalifa Mtukufu anapanga safari kwenda nchi tofauiti

Endelea uk. 4

BODI YA UHARIRI

Msimamizi: Sheikh Tahir M. Chaudhry - Amir Jamaat, Tanzania.
Mhariri: Mahmood Hamsin Mubiru.
Kompyuta: Abdurahman M. Ame.
Mchapishaji: Sheikh Muhammad Arif
Msambazaji: Mwl. Omar Mnungu
Wajumbe: 1. Abdullah Khamis Mbanga
2. Swaleh Kitabu Pazi
3. Jamil Mwanga.
4. Abdillah Kombo

Makao Makuu - Ahmadiyya Muslim Jamaat Tanzania,
Mtaa wa Bibi Titi Mohammed S.L.P. 376.
Simu 022 - 2110473, Fax 022 - 2121744, Dar es Salaam, Tanzania.
Email: mapenziyamungu@yahoo.com

Bila Umoja hakuna Lailatulqadir

Kutoka uk. 1

na Waislam wawili wakiwa katika ugomvi na Mtume Mtukufu (saw) akaingia shughulini kuwapatanisha kiasi hiki kwamba alisahau tarehe ile maalum. Hadhrat Musleh Mauud (ra) alisema kwamba sio tu kwamba Mtume Mtukufu (saw) alisahau tarehe ile bali kwa hakika utambuzi huo uliondoshwa kwa amri ya Mungu. Siku hizi usiku huo hutafutwa katika yeyote kati ya siku za witri za siku kumi za mwisho wa ramadhani.

Hadhrat Musleh Mauud (ra) alibainisha nukta ya muhimu sana kuhusiana na usiku wa hatima. Alisema kwamba kile kipindi kiitwacho usiku wa hatima unahusikana na utungamano (utulivu) wa taifa na umoja. Tunaposikiliza Hadithi tunasema kwamba ingekuwa si ugomvi wa waislam wale wawili tungaliifahamu tarehe maalumu ya usiku huo wa hatima.

Hata hivo fikra kidogo sana inawekwa kwenye jambo hili la muhimu sana ya kwamba saa ile inayoitwa usiku wa hatima inahusikana na utungamano (utulivu) wa taifa na umoja na inaondoshwa kwenye taifa linalopoteza utungamano (utulivu) na umoja. Inasikitisha kwamba nchi nyingi za Kiislam hazina utungamano (utulivu) wowote wala umoja, wananchi wanapigana na wananchi wenzao au wanapigana na watawala au watawala sio waadilifu na ni wakatili kwa raia ukatili unafanywa na kuendekezwa. Kwa sababu ya hali hii iliyoko ndani ya mataifa ya Kiislam, mataifa mengine yanakuwa huru kuyatendea kwa dhuluma mataifa ya Kiislam vyovyote yapendavyo.

Hii ndio sababu Waisrael wanaendelea kuwaua bila huruma wapalestina. Ingelikuwa waislam wameungana na kufuata njia ya Mungu, kwa nguvu kubwa waliyonayo, unyama huu usingefanyika. Ziko sheria na kanuni za vita. Wapalestina hawana nguvu za kuikabili Israeli. Kama ikisemwa kwamba Hamas pia inawatendea ukatili Waisraeli basi nchi za Kiislam inabidi ziwazuie Hamas kufanya hivyo. Mashambulizi baina ya nchi mbili hizi mfano wake ni kama mtu mmoja anapigana kwa fimbo wakati mwenzake anatumia mizinga. Nchi za Kiislam zinafikiri kwamba kama ambavyo hali ya Palestina iliombolezwa Uturuki hivi karibuni, basi wanaamini kwamba kwa uombolezaji rasmi walioufanya wametimiza wajibu wao tayari. Mataifa ya Magharibi nayo hayatimizi wajibu wao. Kilichokuwa kinahitajika ni kwamba pande zote mbili ilikuwa zidhibitiwe, zisifanye uvamizi. Sisi Wa Ahmadiyya tunachoweza kufanya ni kumuomba tu Allah Awanusuru wanaoshambuliwa na wasio na hatia, hali kadhalika na amani ipatikane. Mataifa mengine ya Kiislam yanayo machafuko ya ndani ambapo mateso na vurugu vimeenea. Allah na Awape akili na Awawezeshe kuungana vinginevyo hawataweza kutimiza wajibu wao wa kumwabudu Mungu na hawatapata usiku wa hatima. Panapokosekana utungamano (utulivu) baraka ya usiku wa heshima inaondolewa na giza tu ndilo libakialo.

Usiku wa hatima maana yake ni usiku ule ambamo hatima ya mwanadamu inakadiriwa na kuamuliwa vile atavyoshughulikiwa katika mwaka mzima ujao. Kwa kiasi gani atapata maendeleo na kusonga mbele na manufaa gani atayapata na hasara zipi zitamkabili. Maamuzi ya maendeleo ya binadamu (ya kimwili) pia hufanyika katika giza au usiku. Hadhrat Musleh Mauud (ra) alifananisha maendeleo ya kiroho na maendeleo ya kimwili na akasema kwamba Qur'anTukufu inatuambia kwamba maendeleo ya kimwili ya binadamu yanatokea katika mfululizo wa vipindi vya giza. Kama giza la tumboni mwa mama ambamo maendeleo yote ya kimwili yanahakikiwa. Ukosefu wa lishe bora katika kipindi hicho husababisha udhaifu kwa mtoto. Ni ukweli uliothibitishwa kwamba mazingira na chakula cha mama humuathiri mtoto aliye tumboni sana kiasi kwamba watoto wa akina mama wenye wasiwasi hawapati mafanikio ya maana maishani. Lishe bora na mazingira mazuri wakati wa uja uzito yanayo athari yake kwa mtoto na hii ndio maana Islam inakataza akina mama waja wazito kufunga saumu. Yaweza kusababisha udhaifu kwa mtoto.

Matatizo kama talaka pia yanakatazwa wakati wa uja uzito yasishughulikiwe kwa kuwa huzuni yake inaweza kusababisha udhaifu kwa mtoto aliye tumboni. Ndoa ya mama mjamzito pia imekatazwa kwa sababu uamsho wa hisia vilevile waweza kuleta madhara kwa mtoto aliye tumboni. Mume na mke wanafundishwa kuomba ulinzi dhidi ya mielekeo ya kishetani wakati wa uja uzito ili kwamba miito ya shetani ambayo hutiririka kwenye mishipa pamoja na damu iondolewe ili mtoto wao asipatwe nayo. Sharia imelazimisha matunzo maalum katika siku za kukua kwa mtoto katika tumbo la mama. Mfululizo huu wa vipindi vya usiku wa maendeleo ya mtoto vinafikia hadi pale mama anapomnyonyesha. Hivyo wakina mama wanaonyonyesha pia hawafungi saumu. Mtoto hahusikani na dunia katika hatua hii bali humtegemea mama kwa hiyo haimpasi kufunga isije ikawa na madhara kwa mtoto.

Maendeleo ya kimwili na kiroho hutokea katika giza au (usiku). M aendeleo ya kundi la watu hutegemea kujitolea kwao kulikotangulia na urefu wa kipindi chao cha maendeleo ulio usiku wa hatima. Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba kadri mtu alivyompendwa wa Mungu ndivyo kadiri atakavyokabiliwa na majaribu mengi. Tutafakarini kama twayatumia majaribu ambayo Jamaat inayakabili katika baadhi ya sehemu kuwa ni usiku wa hatima kwetu, muda ambao mtu huwezeshwa kufanya maombi zaidi kuliko kabla. Na tunautambua wakati huu wa mafunzo ya kiroho na maendeleo vilivyo! Hata hivyo ikiwa tutaharibu kiwango chetu cha utungamanao (utulivu) na umoja hatutaweza kufaidika na usiku wa hatima. Ikiwa tutastawisha umoja wetu na utulivu kwa nia ya kupata radhi ya Mungu tutapiga hatua mpya.

Sote tuwe nayo nukta hii muhimu sana mbele yetu kwamba tutayavuka majaribu haya kwa mafanikio hapo ndipo kadirio la maendeleo yetu litakuwa sio la kawaida, kwa hakika kadirio litafanywa na Mungu, yeye ndiye Atakayesikiliza maombi na ni Yeye ndiye Atakayetoa usiku wa hatima. Ni muhimu kwamba tuwe tunashikamana na yale yote yaliyo ni msingi wa kupata usiku wa hatima. Pambazuko litokealo baada ya usiku huo pia sio la kawaida. Hizi ndizo kweli ambazo ni lazima daima tuzikumbuke ili tutafute baraka za usiku wa hatima.

Usiku wa hatima ni jina la kipindi kile ambacho hupata kukubaliwa na hakuna kinachoweza kuwa na thamani zaidi kuliko kile kinachopata kukubalika kwa Mungu. Tujitahidini kwa dhabihu zitakazokubaliwa. Waislam kadhalika na makafiri walikufa katika vita vya Badri. Hata hivyo vifo vya makafiri havikuwa usiku wa hatima wakati ambapo ushahidi wa Waislam ulikuwa ni usiku wa hatima kwa kuwa Mungu Aliwatangaza kwamba wamekubaliwa.

Matatizo, majaribu, taabiko ambalo Mungu halitilii thamani juu yake sio usiku wa heshima, bali ni adhabu. Hata hivyo matatizo na majaribu ambayo Mungu huweka thamani juu yake ndio kusema mkosi, mateso ambayo Mungu huamua kuyalipia ni usiku wa heshima. Amekadiria wakati kwa mwanadamu ambapo muhanga wake kukubaliwa. Jamaat Ahmadiyya imekutana na jambo hili na inaendelea nalo. Popote duniani tunapokabiliwa na majaribu na mateso, nyakati hizi ngumu zinatoa habari njema ya pambazuko. Maoteo ya Ahmadiyya yanazaliwa duniani kote, yaani, Jamaat mpya zinaundwa wakati wote ili kupata baraka zaidi za usiku wa hatima twapaswa kuazimia kuimarisha umoja wetu na utungamano na kama kuna nyufa ndani yake popote pale, tutaziba haraka na tutanufaika kikamilifu na baraka za usiku wa hatima kwa kuwa ni onesho la ..... huruma baina yao ..... (48:30)

Juhudi zetu katika Ramadhani zilenge pia katika kuondoa chuki binafsi na utengano ili tuweze kuzipata baraka za usiku wa hatima sisi wenyewe binafsi na ili kwamba tupate fungu letu katika fadhila zile ambazo Allah Amelikadiria kwa Jamaat. Tuwe pia waangalifu kwa kuwa kadri fadhili za Mungu zinavyoongezeka juu yetu ndivyo hivyo hivyo adui anavyoongeza juhudi za kuleta taabu dhidi yetu. Tusidhanie kwamba hali hii itabakia katika nchi chache tu. Moto wa wivu hujaribu kadri uwezavyo kuzuia maendeleo na hili litatokea kila mahala. Hata hivyo, habari njema ya usiku wa hatima inatubashiria kwamba tutaepushwa na matokeo mabaya ya uadui huu na inatubashiria pia maendeleo ya Jamaat. Ilimradi tumeiweka vyema hali yetu sawa na mapenzi ya Mungu tutaipata baraka ya usiku wa hatima. Mwaminio hujitahidi awezavyo na hutamani maendeleo kwa Jamaat yake ya hali ya juu kabisa kulingana na ahadi iliyotolewa na Mungu, kwa kuhusiana kwetu na Masihi Mauud (as) twatakiwa kuzishika njia ambazo Masihi Mauud (as) alitufundisha kwa ajili ya maendeleo na kupiga hatua. Njia hizi zaweza kuelezwa kwa nukta mbili, ambazo zilisemwa na Masihi Mauud (as) kuwa ndio lengo la kuja kwake. Moja ilikuwa ni kumpeleka mtu karibu na Mola wake na ya pili ni kumfanya mtu atimize wajibu wake kwa binadamu wenzake. Hizi ndizo kazi mbili tulizopewa kama amana kukuza kiwango chetu cha ibada na kuondoa tofauti zetu. Haiwezekani amana hizi zinapotimizwa watu wabaki katika hali ya chuki baina yao. Ikiwa tutajitahidi katika hili tutaweza kuelewa maana ya usiku wa hatima. Masihi Mauud (as) alisema sehemu moja; "Kwa binadamu usiku wa hatima ni wakati wa kujitakasa kwake". Hii ndio aina ya usiku wa hatima tunayopaswa kuitafuta.

Jambo la pili ni lile la Ijumaa ya kuagana. Dhana za ajabu ajabu zimejiingiza kuhusiana na jambo hili. Ni fadhila ya Mungu kwamba ametuwezesha kumpokea Imamu wa zama ambae ametuondolea dhana potofu kama ambavyo Muahmadiyya anatakiwa awe ameepushwa na dhana hizi. Wasio wa Ahmadiyya wanaamini kwamba kwa kuhudhuria Ijumaa ya mwisho ya mwezi wa Ramadhani hata sala ambayo mtu aliiacha kwa makusudi katika kipindi cha mwaka huo inasamehewa, na mtu anasamehewa madhambi yote. Baraka zote za Mungu zinachumwa kwa kuhudhuria Ijumaa ya mwisho ya ramadhani. Kwa fikra yao. Mungu Apishe mbali, Umoja wa Mungu, unategemea sujuda zao nne na kwamba wanamfanyia Mungu hisani kubwa kwa kusujudu kwao huko mara nne ambako Mungu apishe mbali kunastawisha Uungu wa Mungu. Ramadhani haina manufaa kwa watu kama hawa na wala usiku wa hatima. Amri za Mungu ni rehema kwa ajili yetu kwa kuwa ndani yake kuna manufaa na faida kwetu. Kuzifuata amri za Mungu sio mzigo ambao tunatakiwa kujaribu kupata visingizio vya kuukwepa. Mtu hutafuta visingizio dhidi ya kuhukumiwa na adhabu. Watu wenye busara hawatafuti visingizio dhidi ya vitu vyenye manufaa. Nani hatamani kupata watoto? Nani hatamani kupata nafuu kutoka katika hali ya ugonjwa, nani hatamani kupata elimu yeye mwenyewe na watoto wake, nani hatamani kwa ajili ya jamaa na wapendwa wake wapate furaha na faraja, nani hatamani heshima na sifa njema kwa ajili ya watoto wake? Visingizio hutafutwa kwa ajili ya mambo yaliyo kinyume cha haya!. Wakati ambapo amri za Mungu na maelekezo yake ni kwa faida yetu wenyewe, tunatakiwa tuangalie amri za Mungu ziwe kwa ajili ya ibada au kwa ajili ya mambo mengine, zote ni kwa faida yetu. Kuiona amri yoyote ya Mungu kama mzigo ni kujinyima mtu mwenyewe baraka.

Tulipewa uhai na Mungu na Aliupangia lengo uhai huu, kama isemwavyo; "Na sikuwaumba majini na watu ila wapate kuniabudu" (51:57). Hii ibada ya watu na majini ambayo inasemwa kuwa ndio lengo la kuumbwa haihusiani na siku maalum au Ijumaa maalum! Inamaanisha kila sala na kila Ijumaa ambayo ni faradhi mbali na nafali ambazo kila mtu huzitimiza sawa na uwezo wake. Kwa kuwa ibada ndio lengo la msingi la kuumbwa kwetu kuna haja kubwa wa kuizingatia hususan kwa vile ni kwa ajili ya faida yetu wenyewe. Umoja wa Mungu upo na utaendelea kuwepo bila kujali ibada yetu, lakini ikiwa tutamwabudu, pamoja na fadhili zake, tutapata

Endelea uk. 4

Bila Umoja hakuna Lailatulqadir

Kutoka uk. 3

pia baraka zake. Yapaswa ikumbukwe daima kwamba imani yetu itakuwa halisi pale tu tutakapotekeleza amri za Mungu. Mwaminio mwaminifu ana uhusiano wa urafiki na Mungu na urafiki ni pande mbili. Marafiki huyafanya maoni yao yaeleweke baina yao kwa uaminifu.

Ukweli huu unatuelekeza kwenye dhana ya kupokelewa kwa maombi. Ikiwa tutashikamana na amri za Mungu kwa uaminifu, yeye pia atatusikiliza. Marafiki wa kweli hawatamani mabaya kwa mmoja wao. Marafiki wa kidunia wasipotamani mabaya baina yao itawezekanaje Mungu ambaye ni mpenda sana na Anayethamini upendo kuliko yeyote atamani mabaya kwa mtumishi wake? Mtu hupata tu rehema na baraka kutoka kwa Mungu kutokana na uaminifu wake wa imani.

Ikiwa rafiki wa kidunia ambaye ni mwaminifu anachukua hatua ambazo zinaonekana zina madhara kwetu, lakini kwa sababu ya uaminifu wake tunahisi kwamba lazima itakuwapo sababu ya maana ya yeye kufanya afanyayo na tunakuwa na yakini kwamba rafiki hakusudii kutuletea madhara. Tunawezaje kudhani juu ya Mungu kwamba atatutia taabuni ikiwa hivi ndivyo ilivyo basi urafiki wetu na Mungu sio wa kweli, au Mungu Apishe mbali Mungu hana sifa za ukarimu na huruma na ni mdhalimu na anaadhibu bila sababu. Bila shaka dhana hii sii kweli na ni potofu. Mungu ni mwingi wa rehema na mwingi wa ukarimu. Hata hivyo, uaminifu wa urafiki wetu unaweza kupotoka, yaweza kuwa ni udhaifu wetu unaotufanya tusistahili rehema zake! Kwa ajili ya hili twahitaji kuzifanyia mazingatio hali zetu na kuzifanya imani zetu kuwa imara zaidi, na kutekeleza amri za Mungu huku tukizitambua kuwa ni rehema na baraka. Tukiwa na fikra hizi kila tufanyalo katika kutekeleza amri za Mungu huimarisha mioyo yetu na amri za Mungu zinaingia moyoni mwetu na kuwa sehemu yetu. Katika nchi zinazoendelea baadhi ya maofisa hutengeneza sheria zao wenyewe juu ya sheria ya nchi na kuwasumbua watu na watu hawataki hata kuwakaribia maofisa wao. Hata hivyo amri za Mungu sio kama zile za Maofisa walio wadhaifu, zenyewe ni chanzo cha rehema. Kila amri ya Mungu huleta rehema na hubakisha nyuma yake baraka zisizohesabika. Nyakati za sala zimewekwa sio ili mtu asali harakaharaka na kumalizana nayo. Funga ya Ramadhani haitakiwi ivuliwe na kutupwa kando kama ibada zingine zitupwavyo kando na watu wengine wanaowazungukeni.

Mwaminio wa kweli anajaribu kuambatana na ibada hizi kwa kudumu. Ikiwa mwaminio wa kweli anasali mara moja tu kwa uaminifu wa moyo basi sala haziwezi kumponyoka moyo wake kwa kuwa ina faraja ya ajabu itakayomfanya apende kusali wakati ujao. Sala haimalizi na salaam ili kuondoka ndani yake, bali salaam hutamkwa kwa kuwa ni amri ya Mungu itamkwe kwa hakika Ramadhani pia haimwachi mwaminio wa kweli. Hadhrat Musleh Mauud (ra) alisema kwamba kwa msemo wa Kiurdu inasemwa kwamba tunaitunza saumu na huu ni msemo mzuri ulioje. Hatuiachii saumu, bali 'tunaitunza' na siku zote inatufanya tuwe wapokeaji wa baraka za Mungu. Hadithi zinasema kwamba pale mwaminio wa kweli anapokosea matendo yake mema yanakuwa kama ngao ya kumkinga kwa ajili yake na kumwokoa kutoka kwenye kuangamia. Hivi ndivyo tunavyotakiwa tulione kila tendo jema, kwamba lapaswa kuwa la kudumu na hatutakiwi tulipoteze! Mtu anaweza tu kufaidika kutoka kwenye jambo linalodumu, kama isemavyo Qur'anTukufu ..... matendo mema yadumuyo ..... (18:47). Hali kadhalika Ramadhaniiliyotumikakufanya matendo mema inatunzika na inadumu, siku za Ramadhani zitapita lakini matendo mema yaliyostawishwa wakati wa Ramadhani hayataifanya roho ya Ramadhani ituondoke. Waaminio wa kweli wanatakiwa wafanye kila tendo jema, '.....matendo yadumuyo'. Ramadhani pia ni ibada na ibada hubaki katika moyo wa mwaminio wa kweli, hivyo hivyo yatupasa tujitahidi kuitunza Ramadhani ndani ya mioyo yetu.

Mtume Mtukufu (saw) alisema kwamba mtu afanyapo jambo zuri alama nyeupe huwekwa kwenye moyo wake na afanyapo jambo zuri tena alama nyingine nyeupe huwekwa kwenye moyo wake, anaendelea kufanya matendo mema mpaka moyo wake wote unakuwa mweupe. Kwa upande mwingine akifanya tendo baya alama nyeusi huwekwa kwenye moyo wake na kuendelea hivyo mpaka moyo wake wote unakuwa mweusi. Tujitahidi na kuona daima alama nyeupe zinawekwa kwenye moyo wetu. Ramadhani ni kwa ajili ya kujaza mioyo na matendo mema, inahimiza ibada na matendo mengine mema kwa ajili yetu. Tuzikusanye siku hizi na kuzihifadhi kwenye nyoyo zetu na hakuna mtu anaweza kunyang'anya kitu kilichohifadhiwa moyoni mwa mtu, isipokuwa mtu aachie kitu hicho mwenyewe!

Ijumaa ya mwisho katika mwezi wa Ramadhani haiji ili Ramadhani iondoke. Bali huja ili ikiwa tunataka na tuitumie vyema, tuweze kuitunza Ramadhani katika nyoyo zetu kwa ajili ya siku zote zijazo. Mtume Mtukufu (saw) aliita Ijumaa ni Eid na hadithi zinaonyesha kwamba katika Ijumaa unakuja wakati ambapo maombi hupata upokezi maalum. Tujinufaishe na baraka hii wa Ahmadiyya hawaendi msikitini katika Ijumaa ya mwisho ya Ramadhani kumwambia Allah kwamba wamefurahi kwa kuwa Ramadhani imeondoka, wanaenda msikitini katika Ijumaa ya mwisho kusali katika nyakati zilizobarikiwa ili kwamba ingawa Ramadhani itaondoka ndani ya siku chache zijazo lakini Ee Mola, uhifadhi katika nyoyo zetu roho ya Ramadhani na ibada na matendo mema yaliyofanywa ndani yake yasiponyoke kutoka mioyoni mwetu. Tukishika msimamo huu basi tutakuwa tumefanya matumizi yaliyobarikiwa sana ya siku hiyo. Itakuwa ni bahati mbaya sana kama tukisahau ibada na matendo mema tuliyoyafanya katika mwezi wa ramadhani. Marafiki na ndugu hawafurahii kutengana, mtu hufurahi tu kutengana na adui yake. Hivyo mwaminio wa kweli hawezi kufurahia kumalizika kwa ramadhani. Nani atafurahia kuondoka kwa neema? Ni yule tu mwenye bahati mbaya sana! Leo kila mmoja aombe kwamba Allah Atuambatanishe na siku hizi daima dawamu na isitokee muda wetu wowote ukawepo nje ya ramadhani.

Tunapaswa tutafakari juu ya mzizi hasa wa ramadhani. Hakika yake ni hii, mwezi wa Ramadhani ndio ambao imeteremshwa Qur'an(2:186). M waminio wa kweli anatakiwa auweke uzingativu aliokuwa nao juu ya Qur'anTukufu katika m wezi wa ramadhani, kama ni sehemu ya maisha yake katika mwaka mzima. Qur'anTukufu yabidi isomwe katika mwaka mzima na juhudi ifanywe katika kuitekeleza amri zake. Tunatakiwa tuiteremshe Qur'ankatika nyoyo zetu na kuihifadhi humo ili tuweze kuzipata baraka zake katika kila hatua ya maisha.

Mola Atuwezeshe kuyahifadhi mambo haya mawili ambayo Huzur anatutanabahisha na usiku wetu wa hatima uendelee kutupandisha katika vilele vya juu kabisa vya mafanikio, na atuwezeshe kutambua maana yake ya kweli. Na kile kinachoitwa Ijumaa ya kuagana, ambayo hasa ni Ijumaa ya mwisho ya Ramadhani isiwe ni sababu ya kuiacha ramadhani, bali kinyume chake baraka zake ziwe sehemu ya maisha yetu na tuendelee kutimiza lengo la kuletwa kwa Qur'anTukufu.

Waislam wa Palestina inabidi tuwakumbuke kwa hisia katika maombi yetu, Mwenyezi Mungu Awafanyie wepesi hali yao na kuwaondoa katika matatizo.

Kisha Huzur alitangaza kwamba baadae ataongoza jeneza la ghaibu la Naeemullah Khan sahib aliyefariki tarehe 21July, 2014 katika umri wa miaka 61 huko Kyrgystan na alijaaliwa kutoa huduma nyingi katika eneo la nchi za Asia ya kati. Alihamia katika eneo kipindi ilipohimizwa na Hadhrat Khalifatul Masihi – IV (Rh) kuwa Wanajumuiyya wahamie huko. Alikuwa na biashara yake kule lakini pia aliitumikia Jamaat kwa kiasi kikubwa. Aliwaangalia sana wabashiri wetu katika eneo hili na kila mmoja alikuwa anaipa Jamaat heshima ya hali ya juu. Allah na mpatie ghofira na yeye awe mlinzi na msaidizi wa familia yake.

Jalsa Salana, historia, shabaha na baraka zake

Kutoka uk. 2

na kushiriki katika mikutano yao na pale ambapo Khalifa Mtukufu anakwenda kushiriki mkutanoni,wanajumuiya wa huko wanabahatishwa kumwona Khalifa Mtukufu mbele yao.Tanzania ilibahatika kupokea Khalifa wa Allah mara mbili,mnamo mwaka 1988 alipokuja Khalifa Mtukufu wa nne ra na mnamo mwaka 2005 alipotutembelea Hadhrat Khalifa tul Masih wa Tano Allah Amsaidie kwa msaada Wake maalum.

Jalsa Salana ya Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ina shani yake isiyopatikana duniani kote katika mikutano ya kidunia,hii ndiyo Jalsa ambayo upande mmoja inadhihirisha ukweli wa Hadhrat Masih na Mahdi as kama asemavyo kuwa,Allah Ameyatayarisha mataifa ambayo hivi karibuni yatakuja kuungana na jumuiya hiyo na upande mwingine inatupa nafasi ya kujiimarisha kiimani,tunapoangalia wapendwa wafuasi wa Jumuiya hiyo ambao huwa tayari kujitolea muda wao na mali yao ili waweze kushiriki mkutano huu na umaskini hauwezi kuwa kikwazo katika njia yao,hii inanikumbusha wanajumuiya wenzangu wa nchi moja ya bara la Afrika Magharibi iitwayo Burkina Faso ambao walipopata taarifa ya kuwa Khalifa wa Allah anatarajia kushiriki katika mkutano wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya utakaofayinka mjini Accra nchini Ghana mwaka 2008 basi mara moja wakawa tayari kushiriki katika mkutano huu,wengine walisafiri kwa njia ya mabasi na malori lakini pamoja na hao walikwepo wapendwa wa Masihi wa Muhammad saw amabo walipanga mpango wa kushiriki katika mkutano huu kwa kutumia baiskeli zao,ndugu wapendwa hao ndio wafuasi wa Jumuiya hii ya Allah,taaria hii iliposhamiri hapa na pale baadhi ya waandishi wa habari walifika kushuhudia mandhari haya na kurekodi katika jicho la kamera zao wakiwa na wasiwasi nyingi moyoni mwao ya kuwa,je hao watu wataweza kumaliza safari yao toka Wagadugu Burkina Faso hadi Accra Ghana ilhali baiskeli zao ni mbovu na zingene zinaonekana zikishachoka tayari lakini hao waandishi wa habari walikuwa wakiona sura yao ya kidhahiri na kama wangeweza kuona hali na jazba na imani yao wasingekuwa na wasiwasi hizi.Ujumbe huu ulitoka huko na kufika salama nchini Ghana na kushiriki katika mkutano na kwa kumwona Khalifa Mtukufu mbele ya macho yao wakamaliza kiu yao ilhali machozi yalikuwa yakitirika machoni mwao.Upande mwingine hao waandishi wa habari waliojumuika huko Wagadugu kwa lengo la kuwasindikiza wafuasi hao wa jumuiya,siku ya pili asubuhi waliweka habari hii katika magazeti yao ikiwa na kichwa cha habari BAISKELI MBOVU LAKINI IMANI MADHUBUTI.

Katika mkutano huu watu zaidi ya laki moja walishiriki,wengine walitokea nchi za jirani wakiwa wamepanda mabasi na malori na wengine walisafiri wakipanda juu ya paa la mabasi,licha ya kuwa na barabara mbovu,vumbi kali na njia ndefu walipofika,hao wapendwa kwenye uwanja wa Jalsa,walikuwa na bashasha ya hali ya juu usoni mwao,miongoni mwa hao walikwepo wakulima ambao walianza kujiandaa siku nyingi kabla ili waweze kushiriki katika Jalsa salana na walipolima mashamba yao,wakatenganisha sehemu maalum kwa ajili ya kupata matumizi ya safari kwenda Jalsa,hivyo wakatekeleza agizo la Hadhrat Ahmad as ya kuweka akiba kwa ajili ya matumizi ya Jalsa.

Ndugu wasomi Syedna Ahmad as amefanya maombi mengi kwa ajili ya washiriki wa Jalsa Salana na sisi tunaposhiriki kwenye mkutano,pamoja na kupata Baraka zingine pia tunapata sehemu ya maombi haya ambayo yanatufungulia milango mingi ya fadhila ya Allah.Hivyo basi ewe mwanajumuiya uliosikia Mwitaji aliyeita kwenye imani ya kwamba Mwaminini Mola wenu kwa hiyo umeamini uje na uhudhurie kwenye Jalsa hii na upate Baraka na fadhila za Allah.Allah Akusaidie na Awe pamoja nawe katika safari yako. Aamin.

Majibu kwa Gazeti la Alhudaa

Kutoka uk. 1

Uislamu, au ajifanye hamnazo na kufuata kauli za kiafkani za Masheikh wa Alhudaa zinazopingana na kauli murua za Mtume Muhammad saw.

Waahmadiyya tunashuhudia kuwa hakuna apasaye kuabudiwa ila Allah na tunashuhudia kuwa Muhammad saw ni Mtume wa Allah. Tunasali sala tano. Tunatoa Zaka. Tunafunga saumu ya Ramadhani na tunahiji. Kwa ushuhuda wa Mwenyezi Mungu na Mtume wake, sisi ni Waislamu pasina shaka yoyote. Na anayeuhoji uislamu wa Waahmadiyya, basi huyo analeta mafundisho yanayopingana na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake.

Mtume Muhammad saw alibashiri kuwa zitakuja zama, ambapo watapatikana Masheikh wa umati wake, watakaokuwa wakitoa mafundisho yaliyo kinyume na mafundisho yake, watakuwa na mavazi ya Kiislamu na kuongea lugha ya Kiislamu lakini watakuwa wenye amali zenye kuchukiza, watakuwa ni waovu kuliko viumbe wote, watakuwa ni wenye kuanzisha fitna na fitna hizo kuwarejea wenyewe, watamiliki misikiti mikubwa iliyofurika watu lakini itakayokuwa na miongozo potofu.

Halikadhalika alibashiri kuwa umati wake utagawanyika katika makundi 73, ambapo makundi yote, ukiacha moja tu, yatakuwa yamepotoka na kulazimika kwenda motoni. Na hilo kundi moja la peponi litafanana na yeye na masahaba zake.

Pia aliwaasa Waislamu wa wakati huo washikamane na Jumuiya ya Waislamu itakayokuwa na Imamu mmoja atakayekuwa Khalifa wa Mwenyezi Mungu, hata kama iwabidi watambae juu ya theluji au hata kama wanyang'anywe mali zao zote.

Maagizo haya ya Mtume s.a.w yanaafikiana na ahadi ya Mwenyezi Mungu kwa waaminio, iliyomo ndani ya Qur'an Tukufu, sura An Nur (24:56), ambapo Allah Anasema: Allah Amewaahidi wale walioamini kati yenu na kufanya vitendo vizuri kuwa Atawafanya Makhalifa katika ardhi kama Alivyowafanya Makhalifa wale wa kabla yao na Atawaimarishia dini yao Aliyowaridhia (Islam) na Atawabadilisha kutoka kwenye hofu kuelekea kwenye amani. Wataniabudu na hawatanishirikisha na chochote. Na atakayekataa baada ya hayo (baada ya kuwepo kwa nidhamu hiyo ya Ukhalifa) basi hao ndio wavunjao amri.

Hapa, Mungu Aliye Mkweli wa ahadi, Ameahidi kutufanya Makhalifa kama Alivyowafanya Makhalifa wale wa zamani, ambao baadhi yao, kama akina Daud na Adam, wamethibitika ndani ya Qur'ankuwa ni Makhalifa waliokuwa pia manabii. Sasa yule asemaye kuwa hakuna Khalifa yeyote mwenye cheo cha unabii atakayepatikana baada ya Mtume Muhammad saw, huyo anataka kuivunja ahadi ya Mwenyezi Mungu. Na mtu yeyote yule, hata kama awe mwanazuoni, afundishaye yaliyo kinyume na yale yaliyoahidiwa na Mwenyezi Mungu na Mtume wake saw, hawezi asilan kuwa ndani ya kundi lile moja la peponi, yeye ni lazima anakuwa anajumuika ndani ya yale makundi 72 ya upotofu.

Ndio sababu zipo aya nyingi ndani ya Qur'anTukufu zinazodhihirisha kwa ufasaha,

ujio wa mitume baada ya Mtume Muhammad saw, mojawapo ikiwa ni hii hapa ambapo Allah Anasema:

Allah si Mwenye kuwaacha waaminio katika hali mliyo nayo hadi Apambanue mwovu kati ya mwema, na Allah si Mwenye Kukufunulieni mambo ya ghaib, lakini Allah Humchagua (Atamchagua) kati ya mitume Wake Amtakaye. (3:180)

Hapa aya iko wazi kabisa kuwa upambanuzi wa waislamu wema na waovu utadhihirika kwa kutokea kwa Mtume miongoni mwa Waislamu, na Waislamu wema toka kwenye makundi yote yataungana na Mtume huyo na Kuwa chini ya huyo Imamu mmoja. Na waovu kutoka katika makundi yote wataungana kumkataa, kumkufurisha na kumhesabu kuwa ametoka nje ya Uislamu (61:8) ingawa atakuwa akiwaita kwenye Uislamu wenyewe asilia.

Sasa kama wanazuoni wote wa nchi za Kiislamu wanaungana kuikataa neema ya unabii ulioahidiwa kuja baada ya Mtume Muhammad saw, basi hao ni lazima wawe wale waliojumuishwa ndani ya makundi 72 ya upotofu. Na hilo kundi moja ambalo wameshirikiana kulitenga, kama litakuwa sambamba na yaliyobashiriwa ndani ya bishara za kimbingu, kama lenyewe pekee ndilo litakuwa limechipukia kwa nabii, na kama litakuwa pekee ndilo limefanikiwakuwananidhamu ya Ukhalifa ule ulioahidiwa, basi hilohilo litakuwa ndio lile kundi ambalo Waislamu na wanadamu wote tumeagizwa tuambatane nalo.

Mnamo mwaka 1974, chini ya shinikizo la nchi za Kiislamu, zikiongozwa na Saudi Arabia, mtawala wa Pakistan wa wakati huo, Zulfiqar Ali Bhutto, alianzisha kikao makhsus cha Bunge la nchi hiyo, la kujadili kama Waislamu wa Ahmadiyya wanapaswa kuitwa Waislamu au la. Kiongozi Mkuu wa wakati huo wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Khalifatul Masih III, Hafidh Mirza Nasir Ahmad r.a., pamwe na wanazuoni kadhaa wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, waliitwa kuhudhuria kikao maalum kilichofanyika kwa siku kadhaa ndani ya Bunge la Pakistan, kilichojumuisha masheikh na wanazuoni kutoka madhehebu mengine yote ya Kiislamu walioandaliwa makhsus

kukabiliana kwa majadiliano na wanazuoni wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Kikao hicho kilifanyika chini ya udhibiti mkubwa wa serikali, ikihakikisha hakuna taarifa yoyote inatoka nje ya kikao hicho. ni upande wa serikali tu ndio uliokuwa ukirekodi majadaliano hayo ya kihistoria uliojumuisha madhehebu yote ya Kiislamu yaliyogawanyika katika pande mbili. Upande mmoja ukiwa una madhehebu yote ya kiislamu chini ya uongozi wa masheikh na maimamu tofauti, na upande wa pili kukiwa na dhehebu moja tu la Ahmadiyya lililokuwa chini ya uongozi wa Khalifa.

Mjadala uligota rasmi kwenye kuendelea au kutoendelea kwa neema ya utume baada ya Mtume Muhammad s.a.w., ambapo Masheikh na wanazuoni wote wa upande wa Waislamu wengine ulijaribu bila ya mafanikio, kuthibitisha kuwa hakutakuja Mtume yeyote yule baada ya Mtume s.a.w. wakati upande wa pili wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya ulifanikiwa kutoa uthibitisho usio na shaka yoyote kuwa neema ya utume ndani ya Waislamu itaendelea kupatikana, kwa ushahidi madhubuti uliotolewa ndani ya Qur'anTukufu, Hadithi za Mtume Muhammad s.a.w. na fatwa za wanazuoni mbali mbali wa zama tofauti.

Fedheha ilikuwa kubwa sana kwa masheikh na wanazuoni waliokuwa wakidai kuwa hakuna mtume atakayekuja baada ya Mtume Muhammad s.a. w., kiasi ya kwamba serikali ya Pakistan ilipiga kabisa marufuku kwamba mjadala ule usichapishwe popote pale na adhabu kali ingemshukia mwenye kudiriki kuuchapisha. Baadhi ya wabunge waliohudhuria kikao hicho walikiri kwamba kama mjadala ule ungetangazwa hadharani, basi nusu nzima ya watu wa Pakistan wangejiunga na Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya.

Kilichofuata ni kwamba serikali ya Pakistan ikatangaza kuwa Ahmadiyya ilishindwa katika mjadala huo na hivyo kuthibitika kuwa wao si waislamu na hivyo sheria ikapitishwa na Bunge la Pakistan kuwa Waahmadiyya, kuanzia wakati huo, sio tena Waislamu na haki zao zote za kiraia watabidi wazipate ndani ya wigo wa kutokuwa Waislamu.

Serikali ya Pakistan ikapata shinikizo kubwa sana kutoka kila pembe, ikitakiwa iuchapishe na kuueneza mjadala ule uliokuwa umerikodiwa ili watu wajionee jinsi Waahmadiyya walivyoshindwa. Haikuwa rahisi kwa serikali ya Pakistan kulikubali ombi hilo ambalo lingewafichua na kuwaanika masheikh na wanazuoni wanaopotosha umma kwa jinsi walivyoshindwa kwenye hoja na majadiliano ndani ya Bunge hilo la Pakistan. Ni hivi majuzi tu mjadala huo umeweza kupatikana kwa juhudi zisizo rasmi na kuweza kuenea ndani ya mitandao.

Mjadala huo uliofanyika ndani ya Bunge la Pakistan unaweza kumthibitishia kila mwenye akili na busara kwamba kundi la upande mmoja lilikuwa na dhehebu moja tu lililokuwa chini ya uongozi wa Khalifa na ambalo limekuwa likiiomba serikali ya Pakistan iuchapishe na kuueneza mjadala huo. Wakati masheikh na wanazuoni wa upande wa pili waliowakilisha madhehebu mengine yote ya Kiislamu wakiwa wanaishinikiza serikali isithubutu kuuchapisha na kuueneza mjadala huo, kwa nini? Kwa sababu walishindwa kuyathibitisha madai yao na hivyo kulazimika kufanya juhudi kubwa ya kuwaficha watu hali halisi ilivyokuwa bungeni kwa jinsi walivyokabwa na kushindwa hata kupumua wakivuja jasho ndani ya kibaridi cha viyoyozi.

Siku iliyofuata magazeti kadhaa yakaandika kwenye kurasa za mbele kwa uwazi kabisa kuwa Madhehebu 72 yamewasema makadiani kuwa sio Waislamu. Kwa mwenye akili hilo dhehebu lililotengwa ndilo wanazuoni walilolihesabu kuwa limepotea na kustahili kuitwa kwa nguvu kuwa sio la kiislamu na kuwa ndilo lenye kustahili kuwa kundi la motoni. Kwa hiyo, kwa fatwa yao dhehebu lile moja ndilo la motoni na ndio sababu wakaamua kulitoa nje ya Uislamu na wao madhehebu 72, kujihesabu kuwa ndio wenye kustahili kuitwa na kuwemo ndani ya Uislamu na hivyo kuwa wenye kustahiki kuipata pepo ya Mwenyezi Mungu.

Lakini tukirudi kwenye kauli ya Mtume Muhammad s.a.w. tunakuta kwamba yeye alisema kuwa makundi 72 ndio yatakayokuwa ya motoni na kundi moja tu, lenye Jumuiya ya Kiislamu yenye

Imamu mmoja mwenye daraja la Khalifa ndio litakalokuwa la peponi. Hapa hakuna shaka yeyote kwa mwenye akili na busara kuwa kundi la Ahmadiyya lina uthibitisho usiotetereka wa kuwa kundi lile lililoongoka. Kwa sababu ndilo kundi pekee kati ya makundi yote ya Kiislamu lenye uongozi wa Ukhalifa umeodumu sasa kwa zaidi ya karne moja.

Si ajabu kwa masheikh watoao fatwa zilizo kinyume na mafundisho ya Mwenyezi Mungu na Mtume Wake kuwapotosha wafuasi wao na kuifanya sasa Islam ionekane kuwa ni dini mbaya yenye kuchukiza kwa kuhamasisha ugaidi, ukatili, mauaji ya kinyama, ujahili, ukosefu wa uvumilivu, uzinzi na ukosefu wa haya. Damu nyingi sana ya Waislamu inamwagika sehemu mbali mbali duniani kutokana na fatwa zisizo za kiislamu za Masheikh hao.

Ndio sababu Mwenyezi Mungu Alimtuma mwanzilishi wa Jumuiya ya Waislamu wa Ahmadiyya, Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad a.s., kuja kurekebisha mambo na kuwafanya wanadamu warejee kwenye Uislamu ule tulioletewa na Mtume Muhammad s.a.w. kutoka kwa Mwenyezi Mungu.

Bustani ya Washairi

KITENDAWILI

1. NAANZA langu shairi, kumshukuru Rabuka
   Mwenye mwingi utajiri, mpweke alotukuka
   Kunako zote sayari, katu hana mshirika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

2. Ni ngumu yake safari, hofu, giza na mashaka
   Hata awe yu jasiri, mwenye nguvu kupituka
   Hanayo chembe jeuri, hawezi kunufaika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika.

3. Dunia ina ghururi, mengi yametuzunguka
   Ya shuruti na hiari, pia wingi wa mahoka
   Nchi kavu na bahari, nayo anga kadhalika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

4. Mja aombaye kheri, uovu hatoutaka
   Na mipango ni johari, si vyema kuhangaika
   Namba hii ni dosari, hupati kupumzika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

5. Wendaje nyika na pori, kutwa kucha kuzunguka
   Pasi kukata shauri, mahali utapofika
   Ajaliapo Kahari, Mola wetu msifika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

6. Neno silifanye siri, halikawi kugeuka
   Wala sitowe nadhiri, ukadhania dhihaka
   Itakufika hatari, ujutie kutamka
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

7. Lazima ina kiburi, ni vyema kuiepuka
   Usijione mahiri, bado hujakamilika
   Mja aso na hadhari, vigumu kusitirika
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

8. Naugonga msumari, tama hapa kuandika
   Neno moja nashauri, tupange tunayotaka
   Ituepuke athari, ya mwendo bila mipaka
   Asiyejua endako, hakadiriwi kufika

TUMBO

1. TUMBO u rafiki yangu, tulia nikueleze
   Ingawa kwako machungu, nataka uyachunguze
   Yamenitia perengu, sipendi ujizoeze
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

2. Muhibu wewe mwenzangu, ngoja nikuelekeze
   Una hila ulimwengu, ngoma mbaya usicheze
   Vipikwavyo kwenye vyungu, si shuruti uvimeze
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

3. Ni mengi yake mafungu, vyakula nikudokeze
   Vya nafaka kama dengu, vina wanga nikujuze
   Ni bora tangia tangu, vya nafaka usibeze
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

4. Nakusihi tumbo langu, shibe usiichombeze
   Utaja nitia pingu, maungo uyalegeze
   Yaje hima wanguwangu, maradhi yanilemaze
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

5. Kitambi kina mizungu, tumbo unisikilize
   Wahurumie wanangu, mimi usiniuguze
   Nalipenda umbo langu, siyo mbele uchomoze
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

6. Tamati shairi langu, tumbo siniangamize
   Njaa kuiita kwangu, hajayo uniumize
   Umero wako si wangu, niache nijitulize
   Kula ule kwa kiasi, njaa usiidekeze.

KITANDA

1. RAFIKI yangu kitanda, wimbo ninakuimbia
   Huna linalokushinda, wengi wanakusifia
   Juu wanapokupanda, waanzapo kusinzia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

2. La kwanza hunayo inda, yoyote akutumia
   Hili jambo umeshinda, tunzo nakutunukia
   Heshimayo imepanda, Bara, Hindi, na Asia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

3. Japo cha kamba kitanda, hadhiye imetimia
   Usije ukakiponda, hicho ila kukitia
   Wapo wanaokipenda, ndio khasa asilia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

4. Uchovu ukiniwinda, akili kunikimbia
   Sitopenda kuvurunda, kazi nilojipangia
   Hukitafuta kitanda, chumbani nikaingia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

5. Nikavivua vigwanda, na viatu vyangu pia
   Kisha juu nikapanda, naye nilomridhia
   Yetu shuka ya ubinda, moja twajifunikia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

6. Tama nafunga mkanda, kikomo nimefikia
   Zako sifa zimetanda, katika yote dunia
   Mithili ya ndege kinda, unavyonikumbatia
   Kweli huna mshirika, kwa zako nyingi huduma

Mashairi yote matatu ya juu yametungwa na:

Al-Haj Abdallah Salim Seif Alhabsy
P.O.Box 1840 CODE 111,
Muscat Air Port, Seeb.
Sultanate of Oman

UJANA NA DUNIA

1. Ewe ulo na busara, fikiri bibi na bwana
   Fikiri lilo tohara, na lile lilo dhamana
   Pia fikiri izara, wewe nayo kukutana
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

2. Ujana ni jambo bora, ameupamba Rabana
   Tena umetia fora, ulitendalo hufana
   Basi usia mkora, akiba uweke sana
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

3. Kumbuka jambo dharura, jihimu kuweka zana
   Siyo pato kulipura, kwa usiku na mchana
   Ukitoweka ujura, elewa umekubana
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

4. Hebu zituze fikara, ushike ninayonena
   Akiba kwako sitara, ukiijaza shehena
   Na pia huwa kafara, na shida isije tena
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

5. Ufanyapo biashara, ewe kijana kazana
   Ujihimu kila mara, na akiba kushikana
   Uzee ukikudora, uwe umetulizana
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

6. Kwa kweli si masihara, mwanadamu hutatana
   Kukosa kitu ni dhara, jina hutojulikana
   Au uitwe fukara, uzee mja wa lana
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

7. Ujana hukuzingira, ukangiwa na fitina
   Ukafikwa na majira, uzee ukawa jina
   Basi na wako ujira, wakazi weka hazina
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

8. Kaditamati natuwa, na kalamu kuachana
   Na jina kujitangaza, muheshimiwa Magana
   Mmeda tawi kung'ara, masihi kumtangaza
   Sihadawe na dunia, na dunia ina mwisho

Mwl. Ally S. Magana

ZILZAAL (TETEMEKO)

1 Pindi litapopulizwa, Baragumu la kiyama
Na vyote kudidimizwa, ardhini vikazama
Pasiwe chenye kusazwa, ila dhati ya Karima
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

2 Na litapulizwa tena, watoke makaburini
Waja wataulizana, leo ndio siku gani
Mbio wataongozana, kuelekea ugani
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

3 Anadi mwenye kunadi, kwa sauti tajihiri
Kuwanadia junudi, walio kwenye ghafari
Kwamba tuliwaahidi, malipo yenu akheri
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

4 Watu watachungwachungwa, na malaika shadidi
Minyororo watafungwa, mingi isiyo idadi
Kama waendao nyongwa, hawapati jitihadi
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

5 Hawakukufikieni, mitume wenye upeo
Na kukuhadharisheni, kuhusu siku ya leo
Haya sasa ingieni haya ndiyo marejeo
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

6 Hii ndiyo jahanamu, mlio mwahidiwa
Enyi mliodhulumu, nafisi zenu wafiwa
Humu hamna vitamu, adhabu kisawasawa
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

7 Ndipo watakaposema, walodhulumu nafisi
Ole wenu hii dhima, ni yetu na ibilisi
Leo hatuna salama, kwa yale tuloyaasi
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

8 Kumbe wale manabii, waliosema ni kweli
Tusiende njia hii, kaikataza Jalali
Nakama huyu Masihi, alijitahidi kweli
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

9 Mmekula vya haramu, vingi katika dunia
Na bado mmedhulumu, vya watu mmevamia
Mngeiona kalamu, inavyowafatilia
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

10 Tuwaambiapo waja, msiabudu mwingine
Na wao huleta hoja, atokeze wamuone
Japo iwe mara moja, ndipo tukubaliane
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

11 Walumbao na walumbe, haki ishafika kwenu
Ameshatumwa mjumbe, Mirza kafika kwenu
Sikizeni japo chembe, mnusuru roho zenu
Naapa mtaulizwa, kwa kila mlichochuma

HAMISI MSIMBE
MWANDEGE – PWANI

MKAIDI NA SIKU YA IDI (HOJA)

1 Mhariri hodi hodi, ulingo naja kunena
Ni methali sina budi, ya mkaidi kwa kina
Japo ninajitahidi, sijaambua kuona
Methali yake maana, nahitaji ueledi

2 Eti huwa hafaidi, yule mkaidi mwana
Mpaka siku ya idi, kwake yeye humfana
Nashangaa la kuzidi, kuzidia muungwana
Methali yake maana, nahitaji ueledi.

3 Sijui lake kusudi, mkaidi kwa hazina
Sherehe yake wadudi, afaidi kiaina
Atunukiwe zawadi, nalo la maana hana
Methali yake maana, nahitaji ueledi

4 Muungwana na juhudi, eti akapangwe kona
Akoswe na hata kadi, sherehe katu pangana
Navyo vinywaji baridi, viwe kwake kupishana
Methali yake maana, nahitaji ueledi

5 Nakumbuka imebidi, nayo mengi kushonana
Hadithi zile za jadi, wa mwisho mwanzo kubana
Tuzo yake maridadi, wa kwanza kuonekana
Methali yake maana, nahitaji ueledi

6 Kwa vile mi si gaidi, na kaidi wa hiana
Idi kwangu ni stadi, nashehereka kwa sana
Ila methali yanadi, na unyonge kunikuna
Methali yake maana, nahitaji ueledi

7 Muhoni sina zaidi, beti saba ninatuna
Watunzi fanya juhudi, KICHAPWI jibu ungana
BI JALALA na Abedi, Msimbe, Twaha na Jona
Methali yake maana, nahitaji ueledi

"Poem Juggler"
Master JC Muhoni (Nguvu ya m2 mpya)
S.L.P 10960 MWANZA (0786 - 964992)

Kazema amjibu Bishazo

Kwa jina la Allah Mwingi wa Rehma Mwingi wa Ukarimu

Namshukuru Allah s.w. kwa kunipa afya njema na utulivu wa moyo, kuendeleza majibu juu ya hoja za bwana Bishazo na pia namtakia rehma na amani Mtume Mtukufu Muhamad Mustafa s.a.w.

Leo naendeleza majibu kwa bwana Bishazo kuhusiana na aliyoyaandika katika kurasa namba 3,4 na 5.Ya majibu yake kwa makala yangu no. 6c kuhusu Utume kuwarudisha watu kwenye njia iliyonyooka unaendelea.

Hakika katika ukurasa wa 3 ndipo ilipo Aya iliyomtia ukalamsi ndugu yangu na kuibeba na kuitoa hadharani eti ndiyo inayothibitisha uwepo waNabii Issa bin Mariam a.s hai mahali paitwapo Mbinguni kwamiaka zaidi ya elfu mbili sasa - Ukipata nafasi ya kumhoji, atakwambia tu'kun faya kun bwana' - Mwenyezi Mungu Anapolitaka jambo basi huamuru kuwa basi linakuwa . Hana habari kabisa kuwa kuna mambo ALLAH s.w Hawezi asilani Akayafanya. Mwenyezi Mungu hawezi akakhalifukawaida zake alizokwisha ziwekea msimamo.

Kumbuka Bwana Bishazo katika hadithi moja, Mtume s.a.w alimwambia mtoto wa Sahaba wake mmoja aliyeuwawa vitani kwamba Baba yako alipokutana na ALLAH s.w , basi ALLAH Alimpa hiyari ya kuchagua chochote atakacho na Atampa, basi shahidi yule alichagua kurudishwa tena Duniani akafe tena shahidi . Allah s.w Akamwambia hilo halitawezekana maana Alikwisha pitisha kwamba wafu hawatarudishiwa uhai wao mpaka siku ya hukumu. Na hivyo ndivyo Mwenyezi Mungu Anavyosimamia kawaida Zake.

Kabla sijakujibu kuhusu Aya yako uliyosimamia kushinikiza hoja yako ya uwepo hai sayidna Issa bin Mariam a.s kuimarishia imani yako, nataka nikuweke wazi kuhusu kukimbilia kwako kumnukuu Seyyidina Ahmadi a.s na kujiaminisha kwako kwamba sisi tuliyemfuata hatumjui zaidi yako wewe Bwana Bishazo . Unajitia mwenyewe katika hatari kubwa sana . Jihadhari sana na kuchukuwa nukuu za Wapinzani wa Mtukufu huyu na kuzitumia hadharani, waila siku zote utajikuta unaaibika utakapokuwa unajibiwa na hilo litakuja kukusukuma kwenye kutukana na utasimamisha mjadala huu kwa tendo hilo.

Mtume Mtukufu Muhamadi s.a.w mpaka leo anamaadui ambao humzamia na kumkashifu kashifa kubwa kwa namna unavyoelekea wewe kwa Sayyidina Ahmadi hapo baadae.

Katika miaka ya sitini, nilipokuwa nasoma shule ya Kongwa middle school, shule iliyoachwa na wazungu walipohamia Iringa kwenye shule ambayoleo ndiyo Mkwawa Teachers College, nilikutana na Mwanafunzi mwenzangu mmoja kwa jina Gaitani. Nilimkuta anakitabu kimoja ambacho kiliandikwa kuwa Mtume Muhamad s.a.w. alipofariki, aliwekwa mahali wazi ilinaepae Mbinguni.Watu walipoondoka basi (Mungu Apishe mbali), wakaja mbwa na nguruwe wakamnyofoa nyama za mwili wake na hivyo akashindwa kupaa mbinguni, na ndiyo maana Waislam hawawapendi Mbwa na Nguruwe kutokana na jinsi wanyama hao walivyoufanya mwili wa Nabii wao.

Kitabu hicho kilileta madhara makubwa sana kwa Waislam waliosoma enzi hizo, hasa kwa Wapare, Wasambaa Wasukuma nakadhalika, kwani vijana wadogo wale waliiamini

simulizi hiyo na kwa kuwa baba zao walikuwa wenye imani kama ya Bishazo, kuwa Yesu yu hai Mbinguni, iliwarahisishia kuudharau Uislam na Mtume wake na wakawa Wakristo kirahisi.
Wale wenye umri kama wangu na juu yangu watakuwa baadhi yetu tuliokutana na kitabu kile. Pamoja na mambo mengine, kilileta madhara makubwa kwenye Uislam katika zama hizo.
Sasa tazama maadui wa Mtume wanaweza kwenda kiasi gani kuwatungia mikingano. Mtume s.a.w Anatungiwa kashfa katika ndoa zake, katika vita zake n.k. Lakini Bishazo Utukufu wa Mtume s.a.w si bayana kwako? Je nani unaweza kumfananisha nae kwa uadilifu katika kila jiha za maisha ya Mwanadam? Lakini wapo wenye kumzamia mpaka leo.

Shika hadhari yako bwana Bishazo.Ukitaka kuujua Ukristo, nenda kwa Padri atakufundisha Ukristo, na ukitaka Uislam basi nenda kwa Sheikh. Fanya hivyo pia kwa jumuiya zake.Mimi sintotaka kujibizana nawe kuhusu unayoyanukuu kutoka kwa Seyyidna Ahmad a.s.,aliye mwana mtukufu wakwanza wa Mtume s.a.w.Kwakuwa nukuu zako nizakiupinzani wa namna ile ya wanaomzamia Mtume Mtukufu s.a.w. na katika mjadala nikalazimika kuondoka ulipo kama tulivyoamriwa na Qur'anTukufu.

Sasa naanza kujibu hoja yako ya msingi kutoka aya 4:160 ingawa hata itabidi nianzie mbali ili upate kuelewa na usiwe na hoja tena juu ya hili.

4: 160 Na hakuna (kundi lolote) katika watu wa kitabu ila watapatikana watakaomuamini kabla ya kifo chake,
naye (Masihi) siku ya Kiyama atakuwa shahidi juu yao.

Kwaufupi jibu langu kwa hoja yako lipo katika fungu hilo hilo ambapo aya hiyo inapatikana

.Mara kadhaa Mwenyezi Mungu Amesema katika kitabu chake Qurani Tukufu mwisho wa yote ni yeye na Manabii wake ndio huibuka kidedea.

Baada ya tukio la msalaba na kudhania kwao kuwa wamemuua Masihi Issa bin Mariam na hapo basi kaziyake haikufanikiwa au iliishia pale. Mwenyezi Mungu Anatwambia hapana, kazi yake iliendelea na Wayahudi wa makabila yote 12 na madhehebu yote 72 walifikiwa na ujumbe wake, wakiwemo wale wa mataifa kumi waliotawanywa na mfalme Nebukadnezar katika nchi za Mashariki na kulowea huko na kufika hata kwenye miinuko ya Himalaya ya huko Kashmiri ambako Isa a.s. ilibidi awafuate huko baada ya kusalimika na kifo cha msalaba na kuwafikishia ujumbe wake, ambao ulipokelewa na watu kutoka kwenye makabila yote hayo kumi na madhehebu zao, ambapo wako walioamini kikamilifu na wapo walioamini kidogo.
Mpimaji wa imani ni Mungu Mwenyewe, lakini katika kipindi cha miaka zaidi ya 75 ya maisha yake baada ya tukio la msalaba, aliweza kukamilisha kazi yake aliyotumwa na Allah s,w. Na siku ya kiyama atakuwa shahidi mkamilifu kwao kwamba aliwafikia na kuwafikishia ujumbe.

Qur'aninatwambia kuwa Wakristo na Mayahudi watakuwepo mpaka siku ya kiyama:
[.....Na Tutawafanya wale waliokufuata (ewe Isa) wawe juu ya waliokufuru hadi siku ya Kiama.....] 3:56.

Sasa kudhania kuwa eti atakuja Masihi Mwana wa Mariam kuwatia watu wote wa kitabu kwenye Uislam, itabidi tulazimishwe kuamini kuwa Mayahudi wote na Wakristo, hata wale waliokwisha kufa, watafufuka na kumuamini Yesu. Hata mtoto mdogo hawezi kuikubali maana hiyo ya akina Bishazo.

Kwa ufupi pia, jibu la upaaji lipo katika fungu hilo hilo ilipo Aya hiyo.Mlima ulinyanyuliwa juu yaWayahudi hao na kwa hakika umenyanyuliwa hivyo mpaka leo. Mlima huo hauzungumziwi bali unyanyuliwaji wa Issa bin Mariam a.s. ndiyo hoja. Tukio la kunyanyuliwa mlima naona lingekuwa jambo la kihistoria na watu tungefika kuiona sehemu hiyo ulipotoka au kunyofolewa mlima huo. Sasa watu makini tunahoji kwa nini kunyanyuliwa kwa Issa bin Mariam a.s. kuwe si wakimajazi kama ulivyonyanyuliwa mlima bali uwe wa kihalisia?
Ndugu Bishazo!zitafakari dokezo hizo mbili katika vifungu hivyo vichache, ambazo kwa hakika zimelenga kukufikirisha na kukutayarisha juu ya nini kinafuata katika makala ya mwisho. Lakini wenye kuelewa kawaida za Allah s.w.Alizokwisha bainisha katika vitabu vyake, watakuwa wamekamilikiwa na jibu, lakini nitaendelea sasa kutoa ufafanuzi kwako, bwana Bishazo, ili kukuweka wazi na ubainikiwe na jinsi hayo yaliyodokezwa katika paragraph hizo mbili yanavyoungana na kukutoa nje kwenye mwanga. Kuruani Tukufu imetoka Kwa Mwenye Nguvu, Jabbaar, Aliim na Azizi . Wala haina mambo ya kiuganga wa kienyeji au ya kihekaya zaalfu lela ulela ndani yake.

Katika makala unayosema ulikuwa unanijibu,unayo pia nafasi ya kuwaeleza watu na kuonyesha unavyozijali Aya za Mwenyezi Mungu, kwa kuwafafanulia, pale aliposema;
Wale wote wanaoabudiwa kama miungu ni wafu si wazima na hawajui watafufuliwa lini, kwamba wakati inashuka Qur'anhii, je Yesu, wakati huo hadi leo, haabudiwi kama mungu? anaikwepaje aya hii isemayo kwa uwazi kabisa kwamba wale wanaowaita badala ya Mwenyezi Mungu hawaumbi chochotewakiwa ni wafu wasiojua lini watafufuliwa (16:21-22).
Sehemu nyingine Mungu Anatufichulia kuwa wakati Qur'aninateremka watu wa Isa tayari walikuwa wameshaanza kumuabudu Isa kama mungu pale Aliposema;

....Hakika wamekufuru wale waliomsema Masihi mwana wa Mariamu kuwa Mungu..... 5:18.

Sawa na aya hii hata Isa a.s. ni mfu, hayuko hai popote pale na wala hajui lini atafufuliwa.
Kuna bwana fulani tuliwahi kujadiliana, naye akatoa hoja kuwa aya hii haimhusu Isa a.s. kwa kuwa hakuwepo duniani. Nilimuuliza wapi pameandikwa waliopo mbinguni hawahusiki, na kama kuna viumbe vifavyo vinavyoabudiwa kama miungu mbinguni navyo haviwezi kukwepa aya hii pia.

Unatakiwa pia uwaeleze juu ya aya katika makala ile kuwa Anapotajwa Issa bin Mariam kwa namna ya mfano ndipo watu wako wanaupigia kelele mfano huo na utoe hoja zako kwa namna ipi wewe binafsi huhusiki katika kundi hilo la wanaopiga kelele ukiwa unatokana na watu wanaojinasibisha na Muhammad s.a.w.

Kwa mujibu wa Bwana Bishazo Nabii Issa Bin Mariamu a.s yuko Mbinguni, tena akiwa hai na kiwiliwili chake cha udongo. Na kwa jinsi nilivyomuelewa, atakuwa hadi sasa bado tu anaendelea kulala kwa miaka zaidi ya 2000, bila ya kupata athari za matokeo ya kutokula na uchovu usio mithilika kwa kukosa mazoezi.
Lakini ukweli ni kwamba, hakuna katika historia mtu yeyote aliyemuona Yesu a.s akipaa. Ushahidi wa kumuona akipaa hamna katika Kuruani Tukufu na wala katika Biblia Takatifu.
Hilo neno la Yesu kupaa lilibuniwa na wafuasi wake, tena kwa kutumia msaada wa hongo, ili Nabii Issa a.s asiendelee kutafutwa na askari wa serikali iliyokuwepo. Yesu aliishi Palestina kwa muda wa siku arobaini baada ya tukio la Msalaba, kwa kujificha, huku akiendelea kupona majeraha yake ya jaribio lile la Kusulubishwa. **(Mtu haitwi kanyongwa, kachinjwa, kasulubiwa na au kafa maji mpaka kifo kweli kitokee kwa moja ya yoyote katika njia hizo).**
Wa maa swalabuuh, maana yake ni tu kwamba jaribio la kumsulubu kweli lilifanyika, lakini hakufa pale msalabani, na kwa maana hiyo hakusulubika, Allah s.w Alimfananisha tu kama maiti. Kuhusu tukio hili Mwenyezi Mungu katika Kuruani Tukufu Amesema:-
Kur 3 :55
Na Mayahudi walifanya hila na Mwenyezi Mungu Akafanya hila, Na Mwenyezi Mungu Ndiye Mbora wa wafanyao hila.

Hila Aliyoifanya Allah s.w SIYO KUMKIMBIZA Nabii wake Mbinguni kama vile Anawaogopa wale Wayahudi **bali Aliwazubaisha tu wale Wayahudi**. Mtume Mtukufu s.a.w alipokutana na hatari kubwa ya namna hiyo Walipokuwa na seyyidna Abubakari r.a Jinsi walivyotoroka na walipokuwa katika pango la Thaur Mwenyezi Mungu Alitumia maneno namna hiyo kuelezea kushindwa kwa makafiri wale wa Maka :-
Kur 8:31
Na (kumbuka) walipokufanyia hila wale waliokufuru ili wakufunge;

Endelea uk.8

Kazema amjibu Bishazo

Kutoka uk. 7

au wakuuwe au wakufukuze; ***na wakafanya hila na pia Mwenyezi Mungu Akafanya hila, na Mwenyezi Mungu ni Mbora wa wafanyao hila.***

Hila Aliyoifanya Mwenyezi Mungu, ni katika Jinsi Mtume alivyopita mbele ya maadui na kuibuka kwa Tandabui na njiwa wale tunaifahamu nayo pia ilikuwa **ni kuwazubaisha tu wale makafiri.**

Baada ya kupata nafuu alijitayarisha kuondoka kuwaendea kondoo waliopotea wa nyumba ya Izrael, waliopelekwa mateka upande wa Mashariki ya Palestina mnamo mwaka 387 BC na Jemedari wa mfalme Nebkadnezar. Uhamisho ule na kuhilikishwa kwa mji wa Jerusalem, ilikuwa ni adhabu kwa wana wa Izrael kwa matendo yao mabaya ya kumwasi Allah S.W. Matendo yao yalikuwa mabaya hivi kwamba hatahuwezikuyanakili hapa. Kuwahusu Kondoo hao Yesu alinukuliwa akisema:-

Yohana 10:16

na kondoo wengine ninao, ambao si wa zizi hili na wao nao imenipasa kuwaleta na sauti yangu wataisikia kisha litakuwepo kundi moja na mchungaji mmoja.

Huko upande wa Mashariki ndiko yalikopelekwa makabila 10 kati ya 12 ya wana wa Izrael, wakati ule wa uhamisho mwaka 386 BC, na ndipo wakati Nabii wa uhamisho, Nabii Ezekieli, alipooteshwa ndoto ya jinsi alivyoiona Jerusalem iliyoharibiwa NA AKAKATA TAMAA KAMA MJI ULE UTAKUJA KUFUFULIWA LINI.

Allah s.w Akamjulisha kwa Ruya na kuona kwamba mji ule utafufuka tena mnamo miaka 100 tu baadae.

Kur. 2:260

Au kama Yule aliyepita karibu na nji uliokuwa umeangamia : Akasema Mwenyezi Mungu Atauhuisha lini Mji huu baada ya kufa kwake? Basi Mwenyezi Mungu Akamfisha kwa Miaka Mia kisha Akamfufua. Akasema umekaa muda gani? Akasema nimekaa siku moja au sehemu ya siku.(Mwenyezi Mungu), Akasema bali umekaa miaka mia nawe tazama chakula chako na kinywaji chako havikuharib

Nabii Ezekiel ndiye wa kwanza kutumwa kwa wana wa Izrael waliohamishwa na mfalme Nebukadnezar, ambaye ndiye aliowahamisha na kuushushia maangamizi mji wa Jerusalemu. Ni kawaida ya Allah s,w kumpeleka Mwonyaji kabla Hajawaadhibu watu

kur: 17:16

Anaeongoka, basi anaongoka kwa ajili ya nafsi yake tu; na anaepotea basi anapotea kwa hasara (ya nafsi) yake. Wala hatabeba mbebaji mzigo wa mwingine.

Nasi si waadhibishao mpaka Tumepeleka Mtume

Sasa watu wajiulize na hasa Bishazo, vita kuu mbili zilizopita, na ya tatu huenda iko tu nyuma ya pazia, hizo zilikuwa ni adhabu kutoka kwa Allah s.w na Je, kulikuwa na Mtume gani kabla tu ya vita hizo? Mtume, aliyekuja kuishindisha dini ya Allah japokuwa washirikina wa zama hizi wakirihike? Bishazo unaijali vipi Aya hiyo hapo juu? Na je haikutii ukakasi hata kidogo kwamba, Allah S.W. na Issa bin Mariam hai wakiwa mbinguni ni ushirikishaji pia. Wakati sisi tunakwambia Issa bin Mariam a.s wa mfano wake keshafika na wewe kama ilivyotabiriwa katika, Qur'anTukufu waendelea kupiga kelele na unakirihika, mpaka ukaamua kushika upanga wa siku hizi, kalamu? Tafadhali rekebika na umwombe msamaha Mola wako kisha ufuate mwongozo katika njia iliyonyooka. Samahani msomaji kwa kutoka nje ya mada kidogo na kuteta na bwana Bishazo.

Sasa tuendelee na nukuu chache kutoka kwa Nabii Ezekiel za kututhibitishia juu ya kuwepo kwa wale Waizraeli waliosambaa upande wa Mashariki na kufika mpaka nchi ambayo leo hii ni Afganistan na Kashmiri.

Ezekiel 3:4

Akaniambia mwanadamu, haya waendee wana wa Izraeli ukawaambie maneno Yangu –maana wewe hukutumwa kwa watu wa maneno mengine ama wa lugha ngumu bali kwa nyumba ya izrael.

Ezekiel 3:15

ndipo nikawafikia watu waliohamishwa huko Tel-abibu waliokuwa wakikaa karibu na mto kaberi (kabul) nikafika huko walikokuwa nikakaa huko miongoni mwao muda wa siku saba, katika hali ya mshangao mwingi.

Huko basi kama alivyotumwa Nabii Ezekiel na kuwafikia ndivyo alivyotumwa Nabii Issa a.s. Na kwa kweli tunaambiwa ndani ya Qur'anyeye ni Mtume kwa Wana wa Israeli, basi usingetimia Utume wake bila kuwafikia wale 10 kati ya 12 ya mataifa ya Wanaisraeli. Kwa hiyo na akawafikia baada ya tukio la msalaba na Kuruani Tukufu inatueleza juu ya safari hiyo kama ifuatavyo:-

Kur:23:51

Na tulimfanya mwana wa Mariam na mama yake kuwa ISHARA, na tuliwaookoa na tuliwasaidia kuifikia nchi iliyoinuka, mahali penye starehe na chemchem za maji yanayotembea.

Mwanzoni mwa makala hii nilianza kwa kusema hakuna hata mtu mmoja aliyemuona Yesu akipaa na naona ni vyema kulithibitisha hili ili Waislam na hata Wakristo wafahamu kwamba kupaa kwa Yesu ILIKUWA NI TENGENEZO LILILOBUNIWA na wafuasi wake Nabii Issa a.s kwa mintarafu ya kuzuia harakati za kuendelea katafutwa kwa Kiongozi wao na pengine kama Allah Angeruhusu wakamkamata, Mafarisayo (Mashehe wa Wayahudi) sasa wasingefanya ajizi na ndiyo maana neno kumuokoa la Allah s.w katika aya hapo juu limetumika. Mwenyezi Mungu alimtengenezea hali ambapo zaidi ya Plato walikuwepo baadhi ya viongozi wa Mafarisayo waliomwamini kwa siri na hao ndio waliosaidia zaidi kwa maana walikuwa na mamlaka na kwa hiyo ushawishi mkubwa kwa mfano tunasoma:-

Yohana 3:1

Basi palikuwepo na mtu mmoja wa Mafarisayo,

jina Nicodemus MKUU WA WAYAHUDI Huyo alimjia usiku, akamwambia, Rabi twajua ya kuwa u Mwalimu umetoka kwa Mungu.

Sasa ili kuthibitisha kutokupaa kwa Nabii Issa a.s, kwanza nitamnukuu yeye mwenyewe na kisha nitaweka nukuu kutoka kwa wanafunzi wake 2 ambao walikuwa nae siku Yesu anaanza safari yake kuelekea huko ambako leo ndiko nchi za Afganistani Kashimir (Kama Siria) na India. Hawakumwona akipaa bali waliondoka Yeye na Thomas kuwaelekea kondoo wa zizi kubwa ZAIDI huko mashariki.

Nitainukuu Biblia kikamilifu ili msomaji upate picha kamili na ufahamu ya kwamba yaliyoandikwa na Watakatifu Luka, Marko Paulo walioishi miaka 30,60 baadaye, na ambao hawakuwa hata wanafunzi wake, yote yalikuwa maneno ya kusikia tu kutokana na ule uvumi uliovumishwa na pia kuhongwa kwa maaskari wasiendelee kumtafuta mwema huyu .

Nukuu ya Yesu mwenyewe.

(yohana 3:13)

Wala hakuna mtu aliyepaa mbinguni ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni yaani mwana wa adamu.

Tazama kama nilivyoandika katika makala yangu uliyojaribu kujibu, bwana Bishazo, naamini ni kweli nukuu ile hukuipenda, lakini ndio ukweli. Hapa Nabii Issa a.s anataka kuwafikirisha au kutufikirisha:- Hebu tutafakari kushuka kwake kulikuwa kwa namna gani? Si alizaliwa kwa uchungu na kukuwa kama kawaida ya tulivyoshuka mimi na wewe na kama hivyo kupaa kwetu kutakuja kuwa kama alivyopaa yeye kwa Umauti wa kawaida, na ndivyo tulivyoshuhudishwa ukweli huu na Hatamu wa Manabii Muhammad Mustafaa s.a.w.

Mtukufu Mtume wetu S.A.W pamoja na masahaba wake walielewa bila shaka yeyote kuwa Issa bin Mariam alikwisha fariki. Malaika Jibril alimfahamisha Mtume s.a.w kuwa yeye Mtume ataishi nusu ya umri wa Mtume aliyemtangulia. Kwa maana hiyo basi na kutokana na hadithi katika vitabu vya Kanzul Ummal jal. 6 uk. 160 na pia Hujajul Karamah uk. 428 Nabii Issa a.s aliishi miaka 120. Katika muda huo aliweza kuwafikia Wanaizraeli wote wale Makabila 10 yaliyoishi huko na pia katika madhehebu yao 72 aliyoyakuta zama hizo na kuwafikishia na kuwafundisha aliyotumwa nayo kutoka kwa Subhana Wataallah.

Alifariki akiwa amekamilisha kazi yake katika mji wa Srinagar Kashmir na kaburi lake lipo huko. Wanahistoria na Wanasayansi wamejiridhisha juu ya hilo na hata BBC wamekwisha tengeneza documentery juu ya swalla hili. Yesu alikuwa ni miongoni mwa Mitume waliopandishwa daraja, na neno BAL RAFAAHUL LAAHU ILAIHI ni kupandishwa daraja na wala si kubebwa kupelekwa kwa Mungu Mwenyezi **kihalisia** na kiwiliwili kile cha udongo.

Kur 2:254

Hao Mitume Tumewafadhili baadhi yao zaidi kuliko wengine miongoni mwao wako ambao Mwenyezi Mungu Alisema nao wengine wao Akawapandisha daraja na Issa mwana wa Mariamu tukampa Ishara zilizo wazi na tukamsaidia kwa Roho

Lajna Imaillah wapata mafunzo ya Ujasiriamali

Na mwandishi wetu
Dar es salaam

Kinamama wa Kiahmadiyya wapatao 20 walipatiwa mafunzo ya ujasiriamali huko Safina kwenye nyumba ya Jamaat ya Safina iliyoko Wilayani Temeke jijini Dar es salaam.

Kinamama hao walihudhuria mafunzo ya utengenezaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo sabuni za kufulia za maji, na sabuni za mche, sabuni za kunawia mikono, shampoo kwa ajili ya nywele, dawa ya kusafishia vigae pia utengenezaji wa matunda mchanganyiko.

Mafunzo hayo yaliendeshwa na wataalamu wa Kiahmadiyya ambao ni Bi. Tina Mtumbi na Bi. Hija Ayubu ambao pia ni viongozi wa Majlis Taifa. Wataalamu hao waliotoa mafunzo hayo kama sehemu yao ya sadaka kwa wanajumuiyya wenzao na kudhihirisha mapenzi yao ya dhati miongoni mwao kama kauli mbiu ya Jamaat inavyosema; "Mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote".

Baada ya mafunzo hayo Sadri Lajna Taifa Bi. Mwamini Kazema alizungumza na kinamama hao na kuwafahamisha kuwa huu ni mwanzo tu wa mafunzo kwani kuna mafunzo mengine ya vitu vingi yataendelea. Pia akawaomba kina mama wenye ujuzi wa aina yoyote wajitokeze kuwafundisha wenzao kama vile mapishi ya vyakula na kadhalika.

Kwa moyo mkunjufu kina mama hao walidhihirisha furaha nyusoni mwao na kuwashukuru wataalamu hao huku wakisema mafunzo hayo yatakuwa ni hazina kubwa maishani mwao na pia ni msaada katika kujikwamua dhidi ya harakati zao za kila siku za kimaisha.

Waziri wa afya aishukuru Ahmadiyya

Pazi Mazongera

Akipokea msaada wa kisima cha maji kilichochimbwa katika kituo cha afya cha muhoro wilayani Rufiji na Jumuiya Ahmadiyya chini ufadhili wa Majlis Ansarullah Uingereza, Waziri wa Afya Dr. Seif Suleiman Rashid alisema msaada huo ni wa thamani kubwa ukizingatia kuwa kituo hicho kilikuwa hakina maji kwa matumizi ya wagonjwa na wafanyakazi nakuishukuru Ahmadiyya kwa msaada huo aliouita kuwa ni mkubwa sana kwa watu wa Muhoro. Kituo hicho ambacho kinahudumia wakazi wa tarafa hiyo wapatao elfu arobaini kimekuwa kikitoa huduma kwa shida na msaada huo kutoka Ahmadiyya ni mkombozi kwao, alisema MgangaMkuu wa kituo hicho Dr. Suleiman Muhade.

Waziri wa Afya pia aliendelea kuishukuru Ahmadiyya juu ya Msaada mwingine wa maji kwa shule ya Sekondari ya Muhoro kwa kuwekewa pampu mpya ya kisima na kununuliwa matenki mawili makubwa ya kuhifadhia maji. Waziri ambaye pia ni Mbunge wa jimbo hilo la Rufiji alisema kuwa wanafunzi na walimu wa shule hiyo wameanza kupunguza kwa kiasi kikubwa adha ya kutafuta maji.

Aidha Mheshimiwa Waziri alipokuwa anakagua na kupokeakisimakilichochimbwa kwa ajili ya Sekondari ya Ikwiriri alirudia kusema kuwa umuhimu wa maji unaonekana wakati hauna na kwa sasa maji tunayo hivyo tuyatumie kwa uangalifu na kuishukuru Jumuiya ya Ahmadiyya kwa msaada huo wenye thamani kubwa kwa wananchi wa Ikwiriri. Mkuu wa Sekondari alimueleza Waziri kuwa katika bweni la wasichana ambao wamepatiwa kisima hicho kumeondoa hali ya wanafunzi kutangatanga kwa kutafuta maji kwani sasa maji yapo mbele ya bweni lao na matamu ambayo yalionjwa na msafara wote uliofika shuleni hapo.

Mwishoni Mheshimiwa Waziri akimaliza shukrani zake wakati akikagua na kupokea kisima kilichochimbwa kwenye kituo cha Afya cha Ikwiriri alisema Jumuiya ya Ahmadiyya inakaribishwa hapa Rufiji kuendelea kuisadia Serikali katika kuondoa shida na kutoa misaada ya kibinaadamu kama hii. Kituo cha afya cha Ikwiriri kinatoa huduma kwa watu wapatao elfu arobaini wakazi wa Tarafa hiyo na Mheshimiwa Waziri alimuomba mgeni wake Amiri wa Jamaat ya Ahmadiyya Tanzania Sheikh Tahir Mahmood Chaundry wakague pia ujenzi wa Jengo la upasuaji linalojengwa Kituoni hapo. Akijibu shukrani za Waziri wa Afya Amir wa Jumuiya ya Ahmadiyya nchini alisema kwanza anamshukuru Mheshimiwa Waziri pamoja na majukumu mengi aliyonayo ametumia siku nzima kukagua na kupokea visima vya maji vilivyotolewa na Jumuiya Ahmadiyya chini ufadhili wa Ansarullah wa Uingereza. Amir sahib alisema ni jukumu la Jumuiya kusaidia binaadamu na tunalo Shirika letu la Humanity first ambalo limekuwa likifanya kazi hii duniani na hapa Tanzania pia limesajiliwa. Amir sahib alimuombaMheshimiwaWaziri wa Afya kuwa ushirikiano huu uendelee na mapenzi haya miongoni mwetu yadumishwe kwani kauli mbiu yetu ni mapenzi kwa wote bila chuki kwa yeyote.



Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mh. Seif Rashid akipeana mkono na Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry kama ishara ya makibidhiano ya kisima kilichochimbwa na Jumuiya katika shule ya sekondari Ikwiriri.



Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii Mh. Seif Rashid akiongea na wanafunzi katika shule ya sekondari ya Kazamoyo Ikwiriri baada ya kukabidhiwa kisima cha maji safi kilichochimbwa na Jumuiya katika shule hiyo kwa ajili ya matumizi ya wanafunzi na jamii inayozunguka shule hiyo.

kunufaika kupatikana kwa maji hayo na kueleza kuwa Jumuiya ya Ahmadiyya imefanya jambo zito la kuwanusuru wanafunzi kuhangaika kutafuta maji ya matumizi. Akiunga mkono maneno wa Mheshimiwa Waziri wa Afya Mkuu wa Shule ya Sekondari Ndg…… alisema kabla ya msaada huo wanafunzi na walimu walikuwa katika mahangaiko makubwa ya kutafuta maji na walikuwa wakipoteza muda mwingi kutafuta maji wakati mwingine bila ya mafanikio. Takriban wanafunzi wapatao mia mbili pamoja na walimu wao wananufaika na huduma hii kutoka Jumuiya ya Ahmadiyya alisema Mkuu wa Shule hiyo.

Mheshimiwa Waziri wa Afya aliendelea kusema kuwa msaada huu wa kibinaadamu ambao Jumuiya ya Ahmadiyya imetoa ni wa kuigwa na Jumuiya zingine hapa nchini, hayo aliyasema katika tarafa ya Ikwiriri alipokagua na kupokea kisima katika Sekondari ya Kazamoyo kilichochimbwa na Jumuiya ya Ahmadiyya kwa ufadhili wa Ansarullah Uingereza. Waziri aliomba misaada kama hii iendelee na kuendelea kustawisha hali za maisha ya watu hasa walio katika hali ngumu ya maji.

Mkuu wa Shule ya Kazamoyo ambayo ina wanafunzi takriban mia tatu alisema msaada huo umewafanya wanafunzi pamoja na walimu watumie muda wao vizuri kwenye masomo na

JALSA SALANA TANZANIA 2014

Amir na Mbashiri Mkuu nchini anapenda kuwaarifu Wanajumuiya wote kwamba, Jalsa Salana ya Kitaifa mwaka huu itafanyika kwenye siku za Ijumaa, Jumamosi na Jumapili tarehe 26, 27 na 28 Septemba 2014, katika eneo la Jumuiya, Kitonga Dar es Salaam. Inshaallah. Hivyo tunatakiwa kuzingatia yafuatayo:

1. Wanajumuiya wote wajitahidi kuhudhuria Jalsa hiyo na ihakikishwe kwamba kusiwepo hata tawi moja katika kila mkoa ambalo halitokuwa na angalau mtu mmoja atakayehudhuria Jalsa.
2. Masheikh na walimu wajitahidi sana kuwakumbusha wanajuiya juu ya umuhimu na baraka za kushiriki kwenye Jalsa Salana kwa nauli zao wenyewe. Pia kwa vile wanajumuiya wa mkoa wa Dar es Salaam kimsingi hawahitaji nauli ikilinganishwa na wale wa mikoani basi wote wasikose kuhudhuria Jalsa hiyo. Mwanajumuiya wa Dar es Salaam ambaye hatohudhuria Jalsa mwaka huu atatakiwa kujieleza baada ya Jalsa kwa nini ameshindwa kuhudhuria.
3. Marais wa mikoa na viongozi wengine wa Majlis za matawi nao wajitahidi kuhudhuria Jalsa Salana kwa nauli zao.

Jumuiya yasaidia mayatima na walemavu

Na mwandhisi wetu,
Dar es Salaam



Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini Sheikh Tahir Mahmood Chaudhry akikabidhi baadhi ya misaada kwa wakazi wa kituo cha Nungwi kilichopo Kigamboni Dar es Salaam

Siku chache tu kabla ya waislamu duniani kote kukamilisha mfungo wa mwezi mtukufu wa ramadhani, jumuiya imegawa misaada mbalimbali kwa mayatima, walemavu na wafungwa kama sehemu ya kusherehekea sikukukuu ya Eid El Fitr pamoja nao. Misaada hiyo ni sehemu ya jitihada za jumuiya katika kusaidia na kuwahudumia viumbe wa Mwenyezi Mungu.

Akizungumza mara baada ya kukabidhi misaada hiyo katika kituo cha walemavu wa ugonjwa wa ukoma cha Nungwi kilichopo Kigamboni na kile cha watoto Yatima cha CHAUWAMA kilichopo Sinza Mori jijini Dar es Salaam, Amir na Mbashiri Mkuu wa Jumuiya ya Waislamu Waahmadiyya nchini, sheikh Tahir Mahmood Choudhry alisema kuwa: "Tumetoa misaada hii si kwa lengo la kuonesha ufahari ama kujionesha kwa watu, isipokuwa tumefanya hivi kwa kuguswa na hali za ndugu zetu hawa, hivyo tukiwa sehemu ya jamii tumeona ni wajibu wetu kusaidia pale tulipoweza huku tukihamasisha na wengine waige mfano huu".

Wakipokea misaada hiyo kwa nyakati tofauti, wawakilishi wa taasisi hizo, waliishukuru Jumuiya kwa msaada wao na ukaribu walionao kwa jamii hususani wale wenye mahitaji maalumu. Pia, walisema kuwa wamefarijika mno kuona Jumuiya inawakumbuka na kujumuika nao katika kipindi hiki cha sikukuu ya Eid el Fitr.

Aidha, Amir Sahib ambaye katika msafara wake aliongozana pamoja na viongozi kadhaa wa jamaat, aliongeza kusema kuwa, "Uislamu unafundisha waumini wake kuwahudumia viumbe wa Allah hususani masikini na mayatima, hivyo jamaat inatekeleza maagizo hayo kwa vitendo".

Wakati huo huo, akiishukuru jumuiya, mwakilishi wa gereza la keko jijini Dar Es Salaam, alisema kuwa wanaishukuru sana jamaat kwa msaada walioutoa katika gereza hilo huku akielezea kushangazwa na msaada wa ngombe mmoja waliyepewa na kusema kuwa, " hii ni mara ya kwanza kuletewa zawadi ya ng'ombe mzima mahala hapa kwani mara nyingi huwa tunaletewa nyama tu ambayo hatujui namna ilivyochinjwa, hivyo tunafurahi kuwa tutaweza kumchinja wenyewe. Kwa kweli furaha yetu imeongezeka kwa hili.

Misaada hiyo yenye thamani ya zaidi ya shilingi milioni 2.5 za kitanzania, ni pamoja na nguo, sabuni na vyakula.

Itambue Jumuiya ya Afrika ya Kusini

Kutoka uk. 12

langu la msingi ni kutaka tu kusema kuwa hata jumuiya kufikia hapa ilipo, imepita kwenye changamoto nyingi na bado kuna mengi ya kufanya ili Jumuiya iweze kupiga hatua kubwa zaidi za kimandeleo. Na kama Mwenyezi Mungu anavyosema "haibadilishi jamii yoyote mpaka jamii yenyewe iwe tayari kubadilika ....." hivyo kwenye nchi hii nayo haiwezi kwenda kinyume na kanuni hiyo.

Maendeleo ya Jumuiya katika nchi hii ni tofauti na kama wengi wanavyoweza kuwaza, kuwa huenda Jumuiya iko mbali kimaendeleo, la si kiasi hicho, bado jumuiya ni ndogo, ikiwa na wanajumuiya wachache tu. Kama nilivyosema hapo awali, historia inaweza kuwa imechangia kwa kiasi kikubwa uwepo wa hali hii. Unaweza kufikiria tu kirahisi, katika miaka 50 ya Jumuiya, Jalsa kuhudhuriwa na watu 170 ni jambo la kujiuliza kidogo imekuwaje. Lakini ndio hali ilivyokuwa. Ingawa idadi hii kwa hakika ni ya wanajumuiya wanaoishi Cape Town au vitongoji vya karibu na Cape Town, kama vile Paarl, si waliotoka mbali sana na maeneo haya zaidi ya Mbashiri mmoja aliyetoka Swaziland ambako Jumuiya hiyo iko chini ya Jumuiya hii ya Afrika Kusini, alitakiwa afike na mwenzake kutoka Lesotho lakini alikosa Visa ya kuingia Afrika Kusini.

Pamoja na ukubwa wa nchi hii kama nilivyosema, Jumuiya mpaka wa leo iko sehemu chache tu, na kuna baadhi ya maeneo kuna wanajumuiya mmoja mmoja wengi wao wakiwa si wenyeji wa hapa, baadhi ni kutoka nchi za Asia au wengine wamehamia kutoka nchi nyengine za Kiafrika, Ulaya na hata Marekani. Cape Town maarufu kama "Mother City" mji wa mama, ndio makao makuu wa Jumuiya, ambako kuna msikitini wa kiasi si mkubwa sana, ukiwa na sehemu ya juu kwa ajili ya akina mama na chini kwa ajili ya akina baba. Pembeni yake ni nyumba ya Mbashiri Mkuu, maarufu hapa anajulikana kama "Murabbi Sahib" ikijumlisha nyumba yake na familia yake, nyumba ya wageni pamoja na ofisi.

Johannesburg au maarufu kama (City of Opportunity) Mji wa Bahati, ndio mji mkubwa na maarufu wa kibiashara wa nchi hii, kwa hakika Johannesburg kumechangamka sana, kuna harakati nyingi mno za kibiashara na kimaisha kwa ujumla wake, maisha ni haraka haraka mno, pia ni mji wenye idadi kubwa zaidi ya wakaazi. Kijumuiya Johannesburg kuna nyumba moja ya Jumuiya inayotumika kama kituo na sehemu wanajumuiya wanapokutana kwa ajili ya ibada, pia kuna sehemu ya wageni. Nimejaribu kuulizia idadi yao nayo si kubwa ni ya wastani tu si zaidi ya wanajumuiya arobaini kwa ujumla wao.

Pretoria ambako ndio mji mkuu na makao makuu ya serikali, huko hakuna kitu kabisa. Nilisikia kuna mwanajumuiya mmoja au wawili tu, wenye asili ya Asia. Kwa hiyo hakuna harakati zozote za kijumuiya zinazoendelea sana huko. Ingawa si mbali sana kati ya miji hii miwili, Pretoria na Johannesburg ni wastani wa kama kilometa 62 tu.

Darban ni moja ya mji maarufu sana, umaarufu wake haswa umejengwa na kuwepo bandari kubwa katika nchi hii, ni mji wenye harakati nyingi kwa kiasi chake, ukiwa na wakazi wengi wenye asili ya bara Asia, si jambo la kushangaza kabisa kuona hata baadhi ya mitaa ikiwa na majina ya baadhi ya nchi za kiasia. Katika mji huu nako hakuna jumuiya kwa maana ya msikiti au mahali pa kukutania. Ila kuna familia kadhaa, kama si tatu basi nne za wanajumuiya. Hawana mpango maalum sana wa kukutana mara kwa mara, ingawa baadhi ya wakati huwa wanakutana, japo jioni kwa kikombe cha chai na maongezi. Idadi yao si zaidi ya wanajumuiya kumi na watano tu, wanaume, akina mama na watoto.

Kuna eneo la kati maarufu kama Mpumalanga, nimesikia kuna wakaazi wengi wa asili ya nchi hii ambao wamejiunga na Jumuiya, sikupata kujua haswa idadi yao, ila inasemekana ni wengi, hata hivyo sikuwaona kwenye Jalsa. Sikuweza kujua haswa ni kwa nini, lakini ndio hivyo hawakuwepo. Inawezekana swala la "Tarbiyat" linahitajika kwa kiwango kikubwa katika eneo hilo. Nimegusia swala la Tarbiyat kwani ndio msingi wa yote. Kujiunga ni jambo moja, kuelewa kwa nini umejiunga ni jambo jengine, lakini kufuata mafundisho ndio msingi mkubwa zaidi baada ya kujiunga, kinyume chake ni sawa tu na kujaza aina yeyote ya fomu. Ili uweze kufuata mafundisho huna budi kujifunza na kupewa elimu ya jinsi ya kufuata hayo mafundisho.

Najua kwa huku nchi za Afrika mashariki, wanajumuiya hufanya juhudi nyingi ili kuhakikisha wanahudhuria Jalsa, hii inatokana na msingi imara walio nao juu ya jumuiya na kujua umuhimu mkubwa wa Jalsa Salana. Kwa nchi hii ni tofauti kabisa, mfano hii Jalsa ingawa ilikuwa ya kitaifa lakini wengi waliohudhuria ni wakazi wa Cape Town kama nilivyoainisha hapo awali. Kwa hiyo si kama tulivyozoea sana huko nyumbani, watu husafiri kutoka Mwanza, Tabora, Bukoba n.k. ili kuja kuhudhuria Jalsa Kitonga Dar es Salaam.

Utaratibu wa kufanya Tabligh nao ni tofauti kidogo, wengi hufanya tabligh kwa kualika watu tu kuja msikitni au kukutana jioni kwa kikombe cha chai, pia nimeona kwa kiasi kikubwa huku, kumekuwa na ugawaji wa vitabu vya jumuiya, kwenye vyuo vikuu na kwenye maktaba za sehemu tofauti tofauti. Ni utaratibu mzuri lakini ni mgumu sana katika ufuatiliaji. Maana si rahisi sana kujua nani amesoma au pia kujua kama hicho kitabu kimesomwa ama la. Lakini sehemu kubwa hutumika kugawa vitabu na wala sio kuuza vitabu kama tulivyozoea sana katika nchi za Afrika Mashariki.

Uwezo wa kiuchumi si mbaya sana katika nchi hii, ingawa haswa naangalia kwa wanajumuiya, wengi ni watu wenye kazi zao na maisha yao, ingawa bila shaka wanatofautiana uwezo kutoka mmoja na wengine, lakini wengi wao wanajimudu katika maisha yao ya kila siku. Hivyo ni kwa pale tu kunapokuwa na kitu msikitini ndio utaoa watu wapo, kinyume chake si rahisi sana kuona watu wapo tu msikini wamekaa wanapiga soga.

Nimejaribu kwa kiasi fulani tu kugusia na kutoa picha ya hali halisi ya Jumuiya katika Jamhuri hii ya kusini mwa Afrika. Bila shaka yako mengi mengine ambayo sikuweza kuyaandika kwa leo lakini Inshallah pakipatikana nafasi nitajaribu kuona, kujifunza na kuandika mengi zaidi. Najua wao wana mengi ya kujifunza kwetu na bila shaka nasi hatuwezi kukosa cha kujifunza kwao. Na kama tulivyofundishwa kuwa mwisho wa yote mmbora kati yetu ni yule anayefanya juhudi zaidi katika njia ya Mwenyezi Mungu, hali kadhalika inabidi tushindane katika mambo mema, hivyo bado tuna nafasi kubwa ya kufanya vizuri zaidi kwa kila mmoja wetu na kufikia au kupata maendeleo makubwa zaidi ya sio tu jumuiya bali hata ya mtu binafsi.

Mwisho naomba nirejee kusisitiza kwamba lengo la kuandika makala hii si lingine zaidi ya kukupatieni picha kamili ya Jumuiya katika nchini hii iliyo na umaarufu maalum katika bara letu la Afrika. Kubwa linalotakiwa ni kuiombea Jumuiya ya nchi hii na wananchi wake, Allah Awasaidie waweze kupokea mwongozo Wake kwani ni miongoni mwa nchi za Afrika iliyo kwenye mkanganyiko mkubwa sana wa kimaadili na hivyo kuhitaji sana mwongozo wa Kiungu. Mwenyezi Mungu Awasaidie sana.

Amin.

Almasi za Afrika

Kutoka uk. 12

zikiwemo kufunga saumu, kutumia posho kununua vitabu na kuwatembelea masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as) kwa ajili ya maombi na ushauri.

Katika masomo Abdulwahab Adam alikuwa na matatizo makubwa na alisumbuliwa na somo la sheria za Kiislam, na alikuwa na wasiwasi mkubwa juu ya kufanya kwake vizuri katika somo hilo. Tatizo hili alimueleza rafiki yake Amri Abedi ambaye alimtuliza rafiki yake na kumuambia 'usikhofu wala usiwe na wasiwasi'. "Adam mimi ninayo dawa" Alisema Amri. "Acha utani" alisema Adam akimueleza Abedi. Huku akitabasamu Amri alimueleza rafiki yake Adam "Tutakwenda leo jioni kuchimba dawa hiyo". Adamu hakuelewa kwa haraka, lakini alivumilia hadi jioni hiyo ifike ili aone dawa atakayoipata kutoka kwa rafiki yake Amri.

Ikumbukwe ya kwamba toka Amri afike Rabwah alikuwa amejiwekea utamaduni wa kuwatembelea masahaba wa Masihi Aliyeahidiwa (as) ili kufaidika na elimu yao. Mara kwa mara Amri alipenda kumtembelea sahaba maarufu wa Masihi Aliyeahidiwa (as) 'Ghulam Rasul Rajeck' sahaba ambaye alipewa lakabuya 'Redio ya Mwenyezi Mungu'. Yeye akiomba msaada wa Mwenyezi Mungu majibu hayasubiri kesho, bali ni hapo hapo. Hapo ndipo alipompeleka rafiki yake Adam. Walipofika kwa sahaba Ghulam Rasul Rajeck walieleza tatizo lao na mcha Mungu huyu akainua mikono ili kuwaombea. Alipomaliza maombi yake akawaambia; "Nimeona sasa hivi kuwa Masihi Aliyeahidiwa ameweka mikono yake kwenye vichwa vyenu nyote wawili". Taawili yake ni kwamba mtafanya vizuri katika masomo yenu na mtapata heshima kubwa kutokana na kufanya kazi ya Mwenyezi Mungu. Maisha ya baada ya watawa hawa wa kutoka Afrika yalitimiza neno kwa neno ile 'Kashf' aliyoiona mcha Mungu Maulana Ghulam Rasul Rajeck.

Mtihani ule uliokuwa unampa wasiwasi Abdulwahab Adam sio tu kwamba alifaulu vizuri, bali alikwenda maili moja zaidi na kuwa wa kwanza katika darasa lake. Wana bahati mbaya sana wale wanaoendelea kufikiri ya kwamba Mwenyezi Mungu Ameacha kuzungumza na waja wake. Hiyo ni hasara kubwa.

Wote wawili walipomaliza masomo yao ya juu ya theolojia walirudi makwao na kukutanchi zao zikiwa katika vuguvugu la ukombozi. Maombi yale ya sahaba yalipenya hadi katika chimbuko la faraja katika mataifa hayo mawili yaani Ghana ya Kwame Nkurumah na Tanzania ya Julius Nyerere.



Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Osagyefo Kwame Nkurumah enzi za uhai wao

Gold Coast baadae Ghana ikawa nchi ya kwanza kusini mwa jangwa la sahara kupata uhuru wake. Kwame Nkurumah alianzisha chama cha Convention people's party akakiineza nchi nzima ya Ghana na kwa njia ya amani taifa jipya la Ghana likazaliwa mwaka 1957. Na Tanganyika Julius Nyerere akasaidia katika kuanzisha chama cha ukombozi TANU chama ambacho kilipewa mchango mkubwa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya ikiwa ni pamoja na wafuasi wa Jumuiyya hiyo. Kwa amani na kwa kuathiriwa sana na Waahmadiyya kwa mfano kuanza mikutano yao kwa maombi, kufunga saumu mfumo wao ukachukua taswira ya Ahmadiyya wakawa na umoja wa Wazee (Ansar), wakawa na umoja wa akina mama (Lajna) na umoja wa vijana (Khuddam). Tanzim hizo za kisiasa zikafanya kazi kubwa ya kuwahamasisha uma wa wa Tanganyika na maombi ya mfululizo ya Khalifatul Masihi –II, Hadhrat Mirza Bashiruddin Mahmood Ahmad (ra) Tanganyika kwa njia ya utulivu na amani kubwa ikajinyakulia uhuru wake tarehe 09 Disemba, 1961. Sheikh Mubaraka akiwa uwanjani na kufanya maombi. Nani basi anaweza kukataa baraka za maombi ya mteule wa Mwenyezi Mungu sahaba wa Masihi Aliyeahidiwa Ghulam Rasul Rajeck? Na bila shaka maombi hayo yanaonekana katika mkondo wa maendeleo wa nchi hizo. Nchi hizi zikatoa viongozi mashuhuri katika Afrika, Kwame Nkurumah na Julius K. Nyerere. Kama tulivyosema Ghana ikawa nchi ya kwanza kusini mwa jangwa la sahara kupata uhuru wake, na Tanganyika ikawa nchi ya kwanza katika Afrika ya Mashariki kupata uhuru wake. Viongozi hawa wakashughulika usiku na mchana kushughulikia ukombozi na umoja wa Afrika. Itakuwa kichekesho basi kufikiri kuwa mambo haya yote yalitokea kwa ajali. Hapana shaka mwenye jicho linaloona mbali lazima ataona mkono wa siri ambao siku zote hufanya kazi. Ni jicho la yakini tu linaloweza kuona mtiririko wa maombi ya sahaba Ghulam Rasul Rajeck katika mabadiliko hayo yote makubwa yaliyotokea katika nchi hizo mbili yaani Ghana na Tanganyika.

Tukiendelea kuitazama kwa makini taawili ya Kashf ilisema ya kuwa vijan hawa wawili wa Afrika watapewa heshima kubwa. Ni heshima ipi basi anayoitaka binadamu kuliko kusifiwa na Khalifa wa Mwenyezi Mungu? Sheikh Kaluta Amri Abedi alipofariki Mwana Aliyeahidiwa Khalifa wa pili wa Masihi Mauud (as) Hadhrat Mirza Bashiruddin Ahmad (ra) alitamka kuwa; "Wale waliodhani kuwa Waafrika hawawezi chochote, amebadilisha fikra hiyo".

Hotuba nzima ya Khalifatul Masihi – V Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) ya tarehe 26 /06/2014 ilikuwa ni juu ya maisha ya mcha Mungu aliyejitolea maisha yake yote kuwatumikia binadamu wote bila kujali dini au rangi zao. Aliyeonesha utu wa hali ya juu kwa Khalifa Mtukufu, huyo ni mchapakazi Sheikh Abdulwahab Adam wa Ghana.

Wote wawili walijichumia sifa ya kuwa wa kwanza, sheikh Abdulwahab alikuwa wa kwanza kuwa makamu Amir huko Rabwah –Pakistan. Na sheikh Kaluta Amri Abedi alikuwa meya wa kwanza wa jiji la Dar es salaam. Sifa hizi kutimia kwa wale vijana wawili waliomtembelea sahaba Maulana Ghulam Rasul Rajeck hapana shaka humo ndimo kuna chimbuko la mafanikio yao. Na huu ni ushahidi kwa wale ambao bado wana wasiwasi ya kwamba Mwenyezi Mungu (Mungu Apishe mbali) hasemi tena. Tukio hilo ni ishara madhubuti ya kufuta hoja hiyo ya kwamba Mwenyezi Mungu hazungumzi tena.

Mchango wa wana hawa wawili wa Afrika katika uwanja wa elimu ni wa kupigiwa mfano. Sheikh Amri alipopewa fursa ya kuwa Mbashiri wa Dar es salaam alianzisha chuo cha wabashiri kikiwa cha kwanza kuanzishwa na Jumuiyya ya Waislam wa Ahmadiyya nchini. Kazi nzuri iliyofanywa na chuo hicho inaweza kupimwa kutokana na matunda ya chuo hicho. Wanafunzi waliomaliza chuo hicho wametoa mchango mkubwa katika kueneza ujumbe wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Mirza Ghulam Ahmad (as). Juma Mpitakunza, Hassan Mohamed, Awadhi Shoo, Haruni Rashidi Bundara, Mohamed Mkoka na Hamisi Sultani Wamwera ni baadhi ya wanafunzi waliopitia chuo hicho cha wabashiri.

Elimu ya wantanganyika hususan waislam ilimsumbua sana Sheikh Amri. Kwa ujasiri mkubwa alitoa taarifa kwa vyombo vya habari akiilalamikia serikali ya Kikoloni kwa kutowatendea haki Waislam. Waislam kama raia wengine walikuwa wanatoa kodi na kodi hii ikawa inatolewa ruzuku katika shule za Kikristo tu, ambapo waislam hawakuweza kupokelewa. Katika utetezi wake juu ya elimu ya Waislam Sheikh Amri alisema ya kwamba Tanganyika kama ilivyo baiskeli ina mipira miwili na mmoja ukiharibika basi baiskeli haiendi. Mipira hiyo ni Ukristo na Uislam.

Kwa upande ule wa Magharibi ya Afrika Sheikh Abdulwahab alifanya kazi kubwa. Ghana inaongoza kwa kuwa na shule za Sekondari nyingi kuliko Jumuiyya yoyote nyingine katika Afrika. Wanazo sekondari 14, vyuo vya ualimu na masomo ya computer. Lakini linalong'ara zaidi ni chuo cha wabashiri Jamia kinachotoa elimu ya juu. Na huwezi kuzungumzia maendeleo ya chuo hicho bila kutaja mchango mkubwa wa Sheikh Abdulwahab Adam.

Wamchao Rahman ndio wenye mwisho mwema. Ukweli huo ambao umewekwa bayana na Qur'an Tukufu umetimia vilivyo kwa Sheikh Amri Abedi na Sheikh Abdulwahab Adam. Moja ya vitisho alivyovipata Sheikh Amri katika jitihada za kumrudisha nyuma ni tishio la kwamba utazikwa na nani ukifa wewe Qadiani? Sheikh Amri naye hakusita kuwaambia; "Msiponizika nitanuka, na nitaponuka hamtakuwa na njia isipokuwa kunifukia –ndio kuzika kwenyewe". Lakini mambo yakawa kinyume na matarajio ya m aadui wa Mwenyezi Mungu. Mazishi ya Sheikh Amri yalikuwa ya kimataifa. Na taifa lote lilikuwa katika bahari ya majonzi. Rais wa nchi alisikitika kwa kumpoteza mchapakazi mahiri, Kigoma wakampoteza mbunge, Washairi wakampoteza Karii. Ilmuradi wingu la huzuni lilitanda pembe zote. Kana kwamba hiyo haitoshi Amri alizikwa na viongozi wa Afrika Mashariki na ya Kati. Jomo Kenyata wa Kenya, Miltom Obette wa Uganda, na viongozi wa baadae wa Zambia na Malawi walikuwepo. Yaani Dr. Hastings Kamuzu Banda na Dr. Keneth David Kaunda. Ilipigwa mizinga wakati wa mazishi yake na bila kujali itikadi za madhehebu watu walisimama nyuma ya Sheikh Inayatullah Ahmad aliyesalisha sala ya jeneza.

Yaliyotokea Accra Ghana nayo yalitia fora. Ule ulikuwa ni msiba wa taifa zima la Ghana. Maombolezi yalikuwa ni kwa watu wa dini zote. Waliomheshimu Sheikh Abdulwahab Adam ambaye walimsifu kwa kudumisha mapenzi na maelewano. Wanasiasa ambao wanasema aliwapatanisha wakati wa hitilafu zao, mtetezi wa amani, wanafunzi ambao wanapata elimu katika shule za Jumuiyya zilizotapakaa nchini Ghana, rais wa Nchi ya Ghana alitangaza kifo cha Sheikh Abdulwahab Adam kuwa ni msiba wa taifa na jeneza lake lilibebwa na wanajeshi wa jeshi l a Ghana. Hakuna chombo cha Ghana na vingine vya kimataifa ambacho hakikueleza mchango wa Sheikh Abdulwahab Adam katika kusogeza mbele maendeleo ya binadamu. Runinga ya taifa ya Ghana ilionesha mazishi hayo moja kwa moja (live) na ni vizuri ikumbukwe ya kwamba sheikh Abdulwahab Adam hakuwa mwanasiasa bali muhibiri wa dini. Nani basi kwa hivi sasa anaweza kukataa taawili ya Kashf ya Maulana Ghulam Rasul Rajeck kwamba vijana wawili kutoka Afrika watapata heshima. Inatakiwa uwe na moyo wa Thomas au Abu Jahal ambao wote waliona jua linawaka, tena la saa saba mchana na bado wakaendelea kuona giza.

The First Muslim Newspaper in Kiswahili Language since 1936

MapenziyaMungu

Shawwal 1435 AH | Agost 2014 | Zahoor 1393 HS

Kutoka Hadithi za Mtume Mtukufu s.a.w

Imesimuliwa na Hadhrat Abu Said Khudri r.a. ya kwamba Mtume s.a.w. alisema: Jihadi bora ndiyo kusema neno la adili mbele ya Sultani mdhalimu. (*Tirmidhi*)

Almasi za Afrika

Na Mahmood Hamsin Mubiru – Dar es Salaam

Vijana wawili makini kutoka bara la Afrika wakiwa wameelewa vizuri hadithi ya Mtukufu Mtume (saw) 'Tafuteni elimu hata kama ni kwenda hadi Uchina' walifika katika mji wa Rabwa nchini Pakistani mji ambao kwa nje haukuonesha dalili zozote za elimu. Hapakuwepo umeme, bararaba zilikuwa za wasiwasi na ni katika mji huo walipoanza kwa bidii kubwa iliyowashangaza wengi katika kutafuta elimu. Vijana hao wawili mmoja alitoka nchi iliyokuwa inaitwa Gold Coast (Pwani ya dhahabu) kwa hivi sasa ni Ghana na mwingine alitoka Tanganyika ambayo kwa hivi sasa inaitwa Tanzania. Ingawaje walitofautiana kwa umri, wa kwanza akiwa amezaliwa mwaka 1938 na wa pili akiwa amezaliwa mwaka 1924 wote kwa pamoja waliunganishwa kwa pamoja kwa imani yao thabiti juu ya ukweli wa Masihi Aliyeahidiwa Hadhrat Ghulam Ahmad (as) na maisha yao ya baadae yaliendelea kung'ara hadi kupewa lakabu 'Almasi za Afrika'. Vijana hawa ambao wa kwanza alitutoka mwaka 1964 na kutuachia majonzi makubwa, wa pili ametutoka Juni, 2014. Sisi ni wa Mwenyezi Mungu na kwake tutarejea.



Walioketi kutoka kushoto: Sh. AbdulWahhab Adam wa Ghana na Sh. Amri Abedi Kaluta wakiwa kwenye picha ya pamoja na wanafunzi wenzao kutoka Afrika wakati walipokuwa wakisoma Jamia Ahmadiyya Qadiani India.

Maelezo hayo ya juu si riwaya ya kubuni wala mashairi yenye vina, na wala si kitendawili bali ni maisha yaliyotukuka, ya kujitolea, ya imani thabiti na yenye mapenzi yasiyotetereka juu ya Ukhalifa. Kwa mnasaba huo tunazungumzia Sheikh Kaluta Amri Abedi sahib na Sheikh Abudulwahab Adam sahib. Mtu anaweza kujiuiliza unadirikije kuyaleta maisha ya watu hao wawili pamoja? Kama alifanya hivyo Khalifa wa Mwenyezi Mungu – Khalifatul Masihi wa tano Hadhrat Mirza Masroor Ahmad (atba) mimi ni nani n isikanyage pale alipokanyaga Khalifa wa Mwenyezi Mungu?

Ni dhahiri ukitaka kuyaelewa maisha ya mmoja miongoni mwa hao wawili inapendeza kuyalinganisha naya mwingine. Na hapo ndipo utaona muujiza mkubwa wa Mwenyezi Mungu. Kama tulivyokwishasema vijana hao walikutana Rabwa katika harakati za kutafuta elimu, katu hawakupoteza muda wao kama alivyosema Masihi Aliyeahidiwa; 'Muda wa Masihi hautapotezwa bure'. Walisoma kwa bidii na kutumia mbinu kadhaa

Endelea uk. 11

Itambue Jumuiya ya Afrika ya Kusini

Na Abdillah Omar Kombo - Dar es Salaam

Kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, nimejaaliwa kusafiri na kuishi kwa muda katika nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kusini. Ni nchi kubwa yenye utajiri mkubwa wa madini, ina eneo la mraba la wastani wa 1,219,912 kilometa za mraba. Sawa na takwimu iliyofanyika mwaka 2011 ilionyesha hii nchi ina jumla ya watu zaidi ya milioni 41, ingawa kwa sasa inakisiwa kuwa na watu zaidi ya milioni 53, wengi wao wakiwa ni waafrika kwa zaidi ya milioni 40, wazungu zaidi ya milioni 4.5 mchanganyiko zaidi ya milioni 4.6, wenye asili ya Asia na India ni zaidi ya milioni 2.2 na wengineo ni zaidi ya laki 2. Makabila makubwa ya wenyeni ni mawili, Wazulu na Waxhosa, ingawa yapo makabila mengine mengi ya wenyeji na wahamiaji na watu waliochanganya damu.

Kwa fadhila za Mwenyezi Mungu, wakati nikiwa hapa nimefanikiwa pia kuhudhuria Jalsa Salana ambayo ni Jalsa ya 50 tangu jumuiya ilipoingia katika nchi hii zaidi ya miaka 50 iliyopita. Hii ikiwa na maana kuwa miaka hii 50 ni rasmi baada ya jumuiya kupata usajili. Nami kwa fadhila za Allah nilikuwepo kwenye jalsa salana hii ya kihistora ya Jumuiya ya



Masjid Baitul Awwal, Cape Town, South Africa

Afrika kusini kutimiza nusu karne.

Ukilinganisha ukubwa wa jalsa kwa nchi kama Tanzania, Kenya na hata Uganda, jalsa ya hapa ni ndogo sana, waliohudhuria kwa siku zote mbili kwa ujumla ni watu 170, hapo ikiwa ni pamoja na Atfal na Nasrat, hiyo ni idadi ndogo kwa hakika. Najua wengi wanaweza kushtuka kuona idadi hiyo lakini ndio uhalisia wenyewe. Jalsa hapa hufanyika mwezi March tarehe zile ambazo shule zinakuwa zimefungwa. Ni kipindi ambacho hali ya hewa huwa si mbaya, kunakuwa na hali ya hewa nzuri, si joto wala si baridi sana, kwa kawaida si kipindi cha mvua, ingawa Jalsa yenyewe ilifanyika ndani kwenye ukumbi wa chuo cha jamii cha Cape Town.

Nimevutika kuandika na kusema juu ya Jumuiya katika nchi hii, kwa kuwa nimehisi wanajumuiya wengi wangependa kujua juu ya maendeleo ya Jumuiya katika nchi hii kubwa katika bara la Afrika. Ukweli ni kuwa maendeleo yapo ingawa si makubwa sana ukilinganisha na nchi nyengine zilizopiga hatua kubwa zaidi katika maendeleo ya Jumuiya kama Tanzania, Ghana n.k. Ingawa Jumuiya imefika hapa muda mrefu ukilinganisha na nchi nyengine nyingi za kiafrika, lakini huenda historia ya nchi hii imefanya hali kuwa hivyo. Kubwa ni siasa za ubaguzi wa rangi ambazo zimekuwepo hapa kwa muda mrefu mno. Kwa hakika kuna mengi ya kujifunza juu ya siasa hizo na athari zake, na bila shaka athari hizo zitachukua muda mwingi kutoka miongoni mwa jamii hii.

Ni katika hali hiyo hata maswala ya kidini hapa hayana nguvu sana, sisemi kuwa hawana au hakuna dini la, dini zipo na wapo waumini haswa wenye imani za dhati za dini zao, lakini si wengi, wengi wa wenyeji, dini ni kitu cha kufuata mkumbo tu, au niseme ni kama aina ya mtindo. Kwa kuwa wengine wanakwenda basi na wewe unafuata, iwe misikitini au makanisani. Wenyeji wengi bado wanaamini katika dini zao za asili, mizimu na matambiko, si jambo la kushangaza mtu leo akasema ni muumini mzuri wa imani fulani, kisha siku ya pili ukamkuta yuko kwenye ibada ya imani nyengine na siku ya tatu akawa kwenye tambiko na ibada za mila zao za kienyeji au za jadi. Wala si jambo la kushangaza, kuona wenyeji wanashangaa kuona mtu mweusi kuwa nae eti ana dini anayofuata, iwe ya Islam au ya Kiyahudi.

Watu weupe kama vile wenye asili ya bara Arabu, Asia na India, wao moja kwa moja hujulikana kuwa ni Waislam, Wazungu hakuna kuuliza, ni Wakristo tu. Kwa maana hiyo ni wazi kuwa waafrika au watu weusi watakuwa muumini mzuri wa dini za matambiko kuliko dini za kiislam au kiyahudi. Wengi hawajui kuwa yeyote anaweza kuwa muumini wa dini yeyote. Wala si jambo la kushangaza wenyeji kukushangaa wewe mtu mweusi kwa kujiita eti wewe ni Muislam. Uthibitisho wa swala hili alinipa mwanangu Atya, baada ya kuwa na mjadala siku nzima shuleni kwake, ukianza na watoto wenzie, mpaka kwa mwalimu, kuwa yeye si Muislam. Ilibidi basi la shule lisimame kwa muda ili mimi niweze kuthibitisha kwa wanafunzi wenzake kuwa Atya ni Muislam, uzuri ni kuwa Atya mwenyewe alijieleza vya kutosha katika kuthibitisha uislam wake, huku akisoma sura kadhaa za Quran Tukufu kutoka kichwani mwake (Ghaib) hata kabla ya mimi kuhitimisha mjadala huo, kwa kuthibitisha kuwa Atya ni Muislam.

Si nia yangu kuingia sana kwenye mada hii ya imani za kidini katika nchi hii, bali lengo

Endelea uk. 10